

Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo kutoka Bodi ya Ushauri ya Kupambana na Rushwa Afrika (AUABC), iliyowasilishwa na Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Pascoal Joaquim, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa barani Afrika, Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Dk. Nshala uso kwa uso na DCI

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala ametakiwa kuripoti katika ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), kwa ajili ya mahojiano kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kauli alizotoa kuhusu makubaliano ya uwekezaji kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai.

Katika taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi nchini na kusambaa katika mitandao ya kijamii jana, jeshi hilo limeeleza kufanya uchunguzi kauli alizotoa wakili huyo Julai 3, mwaka huu, kuhusu uwekezaji wa bandari na kumtaka afike katika ofisi hiyo asubuhi jana, ili kukamilisha uchunguzi huo wa polisi.

Jana, Nipashe ilimtafuta Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, David Misime, kujua kama Dk. Nshala ambaye alikuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), amesharipoti kwenye kituo hicho, lakini hakupatikana.

Aidha, Nipashe ilimtafuta Dk. Nshala bila mafanikio. Katika mkutano wake na waandishi wa habari hivi, karibuni, wakili huyo alidai kutishiwa maisha na watu ambao hakuwataja akieleza ni kwa sababu ya msimamo wake wa kukosoa makubaliano ya uwekezaji katika bandari kati ya serikali ya Tanzania na Dubai ambao serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikitoa ufafanuzi kuhusu vipengele mbalimbali vya mkataba huo vinavyopigiwa kelele na wadau ikiwamo wanasiasa na viongozi wa dini.

Mwezi uliopita Bunge lilipitisha azimio kuhusu pendekezo la kuridhiwa kwa mkataba baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini baada ya wabunge kupata fursa ya kuchangia na kuishauri serikali kuhusu mkataba huo. Kabla ya wabunge kuchangia, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alipata nafasi ya kuuelezea mkataba huo na manufaa yake kwa taifa.

**LHRC**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeimbusha jamii kutumia uhuru wa kujieleza bila kutweza utu wa mtu mwingine kwa vigezo vya jinsia, jinsi, udini, ukabila, hadhi, ulemavu au rangi ya mtu.

Mkurugenzi wa kituo hicho Dk. Anna Henga, alisema hayo katika taarifa ya kituo hicho, kwa vyombo vya habari ya wito wa kudumisha hali ya uhuru wa kujieleza, jijini Dar es Salaam jana.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alifafanua kuwa takriban juma moja kumekuwapo na mjadala wa baadhi ya Watanzania kulalamika kutishiwa maisha na watu ambao wanawataja kuwa ni wasiojulikana.

Alisema uhuru wa kujieleza unalindwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1989, Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alifafanua kuwa uhuru wa kujieleza pia unalindwa na kuhifadhiwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Dk. Anna alisema ni muhimu hayo yote yafanyike bila kutweza utu wa mtu mwingine kwa vigezo vya jinsia, jinsi, udini, ukabila, hadhi, ulemavu au rangi ya mtu.

# Madudu yaibuka uhakiki wa matumizi kadi matibabu NHIF

**Na Romana Mallya**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umefanya uhakiki wa wanachama na utoaji wa huduma za matibabu kwa wanufaika vituoni na kubaini madudu mbalimbali yakiwamo wanachama kuazimana kadi ili kupata matibabu.

Katika uhakiki huo, wanachama 1,346 wamebainika kuazimana kadi ili kupata matibabu huku zingine 3,589 zikizuiwa matumizi yake.

Kutokana na madudu hayo, NHIF imetangaza kuchukua hatua dhidi ya waliobainika kufanya udanganyifu zikiwamo kusitisha mikataba 48 baina yake na watoa huduma, kuwaripoti watumishi 139 wa sekta ya afya katika mamlaka za ajira yakiwamo mabaraza ya kitaaluma kwa kuzingatia sheria na kanuni.

Pia imesema imesitisha uanachama kwa waajiri 88 ambao ni watoa huduma binafsi na wafanyakazi wao waliobainika kutumia vibaya kadi zao za matibabu kwa manufaa binafsi.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uhakiki unaoendelea kwa wanachama wa mfuko huo. Alisema NHIF imezuia matumizi ya kadi 3,589 za wanufaika zilizokuwa na taarifa zenye shaka.

Alisema pamoja na jitihada za NHIF za kusimamia upatikanaji wa huduma bora kwa wanufaika, bado kumekuwa na changamoto katika utoaji wa huduma, ikiwamo kutozingatiwa kwa masharti ya mikataba baina ya mfuko na wadau wake ikiwamo watoa huduma na wanachama.

"Hadi kufikia Juni 2023, mfuko umechukua hatua hizo kwa waliobainika kufanya udanganyifu. Hatua dhidi ya wanachama wachangiaji na wanufaika 1,197 wa mfuko zimechukuliwa ikiwamo kusitisha matumizi ya kadi 697. Kuamuriwa kulipa gharama za matibabu zilizotumika ni 325 na kuwafungulia mashtaka 67 na kuwaripoti katika mamlaka za uchaguzi ni 108," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema katika kuimarisha usimamizi wa huduma za bima ya afya kwa wanachama na kupata suluhisho la changamoto zinazojitokeza na kuhakikisha kuwa wanapata huduma bora, kuanzia Juni, mwaka huu, mfuko uliweka watumishi wake katika baadhi ya vituo Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Dodoma.

Kwa mujibu wa Konga, tathmini ya jumla tangu kuanza kwa mpango huo, imebaini kuwapo kwa changamoto mbalimbali.

Alisema kwenye matumizi mabaya ya kadi, baadhi ya mambo yaliyobainika ni wanachama kutoa kadi zao kwa wasio wanachama wa mfuko, hivyo kupata huduma kinyume cha sheria na utaratibu.

Katika utoaji wa huduma, alisema NHIF imebaini baadhi ya vituo kutozingatia utaratibu wa uhakiki wa wanachama kabla ya huduma hivyo kuruhusu watu wasiostahili kupata huduma kwa gharama za mfuko.

Pia alisema imebainika utoaji huduma kwa wanufaika wasiofika vituoni au kwa kuwatuma ndugu kuwachukulia dawa.

"Miongozo inaelekeza mgonjwa kuonwa na daktari na si kupatiwa ndugu, jamaa na marafiki. Mfuko umetoa ridhaa kwa watoa huduma kutoa dawa za hadi miezi mitatu ili kuepusha usumbufu kwa wanachama pale anapotoka mbali," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema hatua ambazo NHIF inachukua kukabiliana na changamoto hizo ni kuzuia matumizi ya kadi 3,589 za wanufaika zilizokuwa na taarifa zenye shaka na kuwataka kufika kuhakiki taarifa zao kama ilivyoelekezwa awali na mfuko.

Pia alisema mfuko unafanya uchambuzi wa matumizi ya kadi zote zilizobainika kutumika kinyume cha utaratibu na kuchukua hatua stahiki.

"Kuzuia malipo ya huduma zote za matibabu zilizobainika kuwasilishwa kinyume na utaratibu uliowekwa na mfuko. Kuongeza wigo wa matumizi ya utambuzi wanachama kwa kutumia alama za vidole na sura kwa vituo ya kimkakati ikiwamo kliniki za kibingwa, hospitali za ngazi ya rufani, kanda na taifa," alisema.

Alisema maandalizi yameshaanza kwa kushirikiana na watoa huduma na sasa hatua iko kwenye majaribio na wanategemea kupeleka kwenye vituo vyote ndani ya mwaka huu.

"Kuongeza udhibiti wa kielektroniki katika uhakiki na uwasilishaji wa madai kabla ya malipo," alisema.

HABARI KITAIFA

## Wanaume wadai kurushwa kichura ili kupata unyumba

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

BAADHI ya wanaume katika Mtaa wa Namkuku Halmashauri ya Mji wa Nanyamba mkoani Mtwara, wamelalamikia vitendo vya unyanyasaji vinavyofanywa na wake zao kwa kutowapa haki ya tendo la ndoa hadi watakapotekeleza masharti wanayowapa likiwamo la kuruka kichura-chura kuzunguka kitanda.

Wakiongea jana katika warsha ya uelimishaji kuhusu ukatili wa kijinsia, haki ya afya na hedhi salama kwa viongozi wa mitaa yanayoendelea mjini Nanyamba, mmoja wa viongozi hao alisema wanaume wamekuwa wakilalamika kufanyiwa ukatili na wake zao kwa kunyimwa tendo la ndoa na wakati mwingine kutoa masharti magumu.

"Unaambiwa ili nikupe ruka kichura-chura kuzunguka kitanda, kwa kuwa una shida na hilo tendo basi unaruka...huu ni ukatili wa kijinsia, kesi kama hizi zipo na zinawaumiza wanaume wengi na huenda ikawa miongoni mwa vyanzo vya kuvunjika au kuyumba kwa ndoa nyingi," alisema Joseph Nanyimbula Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Namkuku.

"Wengine wanalazimika kuwatongoza tena wake zao ili wapate tendo la ndoa, yaani ulimtongoza kabla ya kumuoa, ukamuoa na sasa ukitaka haki ya tendo la ndoa unaanza kumtongoza tena, yaani unabembeleza, wengine wanatozwa pesa tena, yaani ulitoa mahari na unapotaka tendo la ndoa unatoa pesa nyingine katika ndoa wanaume tunanyanyasika na hatuna kwa kulalamika."

Alisema akiwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, anapokea malalamiko mengi ya wanaume kunyanyaswa na wake zao hasa linapokuja suala la tendo la ndoa, kwa kupewa masharti au kunyimwa kabisa hali inayoyumbisha ndoa nyingi mtaani hapo.

"Niwaombe wanawake waache huu unyanyasaji, hauna tija kwa ustawi wa familia, zaidi unakaribisha michepuko na kujiweka katika hatari ya kupata maradhi," alisema.

Joel Emanuel ni Mtendaji Kata ya Nanyamba alibainisha kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye kata hiyo vimepungua, licha ya kukosa takwimu bado alisisitiza kuwa jitihada mbalimbali za wadau kuelimisha jamii zimeanza kuzaa matunda.

"Ukatili ambao kwa sasa ni mkubwa ni wa kingono, juzi kuna kijana tumemkamata alimfungia ndani mwanafunzi wa darasa la saba, nguvu zetu tunapaswa kuziwekeza huko ili kulinda maadili ya kitanzania," alisema Emanuel.

Ofisa mradi wa Haki ya Afya unaotekelezwa na Shirika la Smile for Community kwa kushirikiana na wasaidizi wa sheria (paralegal) Mtwara kwa ufadhili wa Legal Service Facility (LSF), Aneth Kiyao, alisema mafunzo hayo yameshirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa na vijiji 66 kutoka halmashauri hiyo.

"Mradi huu upo katika kata tatu za Nanyamba, Nyundo na Ndumbwe, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa kutambua aina ya ukatili wa kijinsia na madhara yake ili kama viongozi waweze kuchukua hatua stahiki pindi wanapokutana na matukio hayo katika utendaji wao wa kazi na kusaidia kuyatokomeza," alisema.

Kadhalika, alisema matukio ya unyanyasaji wa kijinsia hasa ukatili wa ngono ikiwamo ulawiti wa watoto wa kiume na wanaume kulazimisha kuwaingilia kinyume na maumbile wake zao yamekuwa yakiongezeka na ni wajibu wa jamii yote kukemea vitendo hivyo.



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Rogers Sempindu (kulia), akimpima macho mmoja wa waliofika kupata huduma hiyo, kwenye banda la MNH katika Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Utekelezaji agizo la Samia waleta ahueni bei ya mafuta

**Mwandishi Wetu**

MAAGIZO ya Rais Samia Suluhu Hassan yamesaidia kushusha bei ya mafuta ya petroli na dizeli nchini kwa mwezi wa pili mfululizo, huku nchi jirani ya Kenya wakilia na ukali wa maisha unaotokana na kupanda kwa bei hiyo.

Baadhi ya wamiliki wa magari kutoka Kenya wameamua kuvuka mipaka ili kuweka petroli na dizeli kwenye vituo vya mafuta vya nchini Tanzania, ambavyo huuza kwa bei ya chini.

Takwimu za EWURA zinaonesha kuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam, bei ya kikomo ya petroli mwezi wa Julai imeshuka kwa Sh. 137 kwa lita hadi kufikia Sh. 2,736, wakati bei ya dizeli imeshuka kwa Sh.118 kwa lita hadi kufikia Sh. 2,544.

Kwa sarafu ya Kenya, bei ya mafuta ni Sh. 147.96 (sawa na Sh. 2,553.57 ya Tanzania) kwa lita ya dizeli na Sh. 159.13 (2,746.35) kwa lita ya petroli.

Bei halisi ya petroli Kenya ni Sh. 195.53 (sawa na Sh. 3,374.56 ya Tanzania) kwa lita wakati bei ya dizeli ni Sh. Sh. 179.67 (Sh. 3,100 ya Tanzania) kwa lita.

"Madereva wa magari wengi wa Kenya wanavuka mipaka ya Namanga na Sirari na kuja kuchukua mafuta ya petroli na dizeli kwenye vituo vya Tanzania kwa ajili ya unafuu wa bei," alisema Aloyce Mushi, mfanyabiashara wa mafuta, Arusha.

Ahueni ya bei ya mafuta nchini Tanzania imetokana na agizo la Rais Samia kuwa serikali ichukue hatua za kupunguza kupanda kwa gharama ya maisha nchini.

Rais Samia aliagiza kuwa serikali itoe ruzuku ya Sh. bilioni 100 kwenye bei ya mafuta kila mwezi, ili kudhibiti kupanda kwa bei za petroli, dizeli na mafuta ya taa nchini.

Aliagiza pia kuwa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), ihakikishe inadhibiti ushindani wa kampuni zinazoingiza mafuta nchini kwa lengo la kushusha bei.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) nalo limeingia kwenye biashara ya kuagiza mafuta kwa pamoja ili kuleta ushindani kwa kampuni binafsi na kuhakikisha bei ya mafuta inashuka nchini.

Ahueni ya bei ya mafuta nchini Tanzania imeleta manufaa kwenye uchumi na pia kushusha gharama za maisha kwa wananchi wa kawaida.

Mfumuko wa bei kwa mwezi Mei 2023 ulishuka hadi kufikia asilimia 4.0 kutoka asilimia 4.3 kwa mwezi Aprili 2023, kwa mujibu wa takwimu za NBS.

Wakati huo huo, bomba la TAZAMA lililojengwa miaka ya 1960 ambalo lilikuwa linasafirisha mafuta ghafi kutoka Tanzania hadi Zambia, sasa litaanza kusafirisha mafuta ya dizeli kutoka Dar es Salaam hadi Zambia, badala ya mafuta ghafi kama ilivyokuwa hapo awali.

Kwa mujibu wa takwimu za bei ya mafuta zilizotolewa Julai 4, mwaka huu bei ya lita moja Uganda inanunuliwa kwa Shilingi ya Tanzania 3,299.6, Kenya (3,166.9), Rwanda (3,1557.8), Jamhuri ya Kidemokrasi Congo (3,009.9) na Tanzania ni 2,736.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema baada ya kuanza kusafirisha dizeli kwenye bomba la mafuta, hali ya usalama na mahitaji ya usalama ya bomba hilo yameongezeka sababu ni rahisi watu kushawishika kutoboa bomba hilo na kuchukua dizeli.

Makamba alisema kuwa bomba hilo limejengwa muda mrefu na lina kipenyo chembamba, wakati biashara ya mafuta imekua na mahitaji ya ni makubwa zaidi.

Alisema kuna haja ya kujenga bomba pana na jipya litakalosafirisha pia bidhaa nyingine zaidi ya dizeli.

**WANANCHI WAFUNGUKA**

Wachumi na wadau wa usafiri nchini wamesema kiwango cha bei ya petroli na mafuta kilichopungua ni kidogo kuleta unafuu kwa Watanzania hasa wafanyabiashara kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji katika usafirishaji nchini.

Mchumi kutoka Taasisi ya Usimamizi Wajasiriamali na Maendeleo (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema punguzo hilo halijulikani kama litadumu muda kwa muda gani.

Alisema watakaoona manufaa ni wale wanaotumia mafuta moja kwa moja, ikiwamo madereva wa magari binafsi na mabasi ya biashara lakini wanaotumia huduma ya usafiri hawatoona badiliko lolote.

Meneja wa kampuni ya mabasi yaendayo mkoani ya Tashrif, Hamisi Shemweta, alisema kiasi kilichopungua ni kidogo kupunguza gharama za uendeshaji na kuiomba serikali ipunguze zaidi.

Mfanyabiashara wa nguo Kariakoo, Irene Lymo, alisema anaona manufaa ya kushuka kwa bei ya mafuta kupitia usafiri wake binafsi ingawa sio makubwa, lakini hafikirii kama gharama za usafirishaji wa bidhaa zinaweza kushushwa na punguzo hilo kwa kuwa ni dogo.

# Matindi atwaa tuzo ya Mtendaji Mkuu Bora Shirika la Ndege Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Ndege Nchini (ATCL), Mhandisi Ladislaus Matindi, amepata tuzo ya Mtendaji Bora Afrika kwa uendeshaji wa Shirika la Ndege.

Tuzo hiyo ilitolewa hivi karibuni na Taasisi ya Business Executive Institutions ya nchini Mauritius.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Shirika hilo, Sarah Reuben, wakati akizungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa maarufu kama Sabasaba.

Alisema tuzo hiyo ilikabidhiwa kwake wiki iliyopita nchini Mauritius na moja ya vigezo vya kupata tuzo hiyo ni utendaji wake kwenye shirika na historia ya ubobezi wake kwenye sekta ya usafiri wa anga.

Sarah alisema katika kipindi cha mwaka 2016 mpaka 2023, kumekuwa na maboresho mengi ya kuhuisha Shirika hilo la ATCL na yeye amekuwa mstari wa mbele kufikia mafanikio hayo.

"Kwa kutambua mchango wake namna alivyofanikisha mageuzi ndani ya shirika kwa muda mfupi tu kwa kulinganisha na utendaji wa kampuni zingine za ndege wakaona wampe yeye kwa mwaka 2023 ya Mtendaji Mkuu Bora Afrika," alisema.

Alisema miongoni mwa vitu vilivyoangaliwa ni uendeshaji wa shirika, ongezeko la safari za ndege, ongezeko la vituo vya ndege, namna anavyosimamia safari za ndege na namna alivyofanikiwa kupunguza hasara za shirika.

Alisema vigezo vingine vilivyoangaliwa ni namna alivyofanikiwa kuongeza watendaji na wataalamu wa aina mbalimbali ndani ya shirika hilo kama marubani na wahandisi wa ndege.

"Kuna vigezo vingi vinaangaliwa kwa mfano uwezo wake wa kuwasimamia marubani, kusimamia hizi ndege na uwezo wa kufanya matengenezo ya ndani yamechangia kupata hii tuzo ambayo hutolewa kila mwaka na uwezo wake wa kuchangia kwenye masuala mbalimbali ya kikanda," alisema.

Pia, sifa nyingine iliyomwezesha kupata tuzo hiyo kuwa ni mchango wake katika Umoja wa Mashirika la Ndege Afrika (AFRAA) na Mhandisi Matindi ni mmoja wa wajumbe.

"Hii siyo tuzo pekee ambayo amepata kwa mwaka huu kwasababu hivi karibuni pia shirika limepata tuzo kutoka kwa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) inayoangalia ubora wa uandaaji wa hesabu na utoaji wa ripoti waliona ATCL imeandaa vitabu bora vya hesabu wakampa tuzo," alisema.

Sarah alisema miaka ya hivi karibuni ATCL iliwahi kupata tuzo ya kuwa shirika linalotumiwa zaidi kwa hapa nchini kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Hivi karibuni Tanzania iliweka historia ya kipekee kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kununua ndege yake kubwa ya mizigo Boeing 767.

Ndege hiyo iliwasili Juni mwaka huu na kupokewa na Rais Samia Suluhu Hassan na wageni mbalimbali kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) na tayari imeanza safari za nje ya nchi.



Meneja wa Miradi wa Hospitali ya CCBRT, Yohana Kasawala (katikati), akizungumza na waandishi wa habari juzi, kuhusu kambi ya matibabu ya fistula ya uzazi inayoendelea katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi-Sokoine. Wengine ni Dk. Naomi Makota kutoka Kampuni ya Equinor Tanzania (kulia) na Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Alexander Makala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MUHAS ya tatu utoaji elimu bora Kusini Jangwa la Sahara

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), kimeendelea kung'ara katika utoaji elimu baada ya kushika nafasi ya tatu kati ya 121 kwa vyuo vyenye ubora kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Appolinary Kamuhabwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio waliyoyapata.

Alisema ripoti iliyotolewa Juni mwaka huu na Mtandao wa Kimataifa wa Times Higher Education (THE), ilibainisha kuwa MUHAS ni taasisi ya tatu kwa ubora kati ya 121 na nafasi ya kwanza na pili imeshikwa na vyuo kutoka Afrika Kusini.

Profesa Kamuhabwa alisema mafanikio hayo ni matokeo ya mipango ya kimkakati na sera ambazo ziliwekwa na kutekelezwa kwa miaka kadhaa iliyohusisha kuboresha ufundishaji, kujifunza na utafiti MUHAS.

"Ushindi huu una maana gani? Kwanza tunajulikana duniani kwa ubora, pili imeitangaza nchi, tatu inakwenda kuongeza imani kwa wahisani katika kutoa misaada ya kifedha kwa chuo chetu, nne inakwenda kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka nje watakaokuja kusoma hapa kwetu, tano wahitimu wetu wanakwenda kupata soko la ajira," alisema.

Kadhalika, alisema mwanzoni mwa mwaka huu THE iliitambua MUHAS kuwa katika nafasi 10 miongoni mwa vyuo vikuu bora Afrika.

Alisema katika uainishaji huo wa ubora MUHAS pia kilikuwa chuo kikuu cha tano Afrika na kuwa katika kundi la vyuo vilivyo katika nafasi ya 401 hadi 500 duniani.

Alisema MUHAS imepata mafanikio hayo kutokana na utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika mpango mkakati wa chuo.

Profesa Kamuhabwa alisema kwa sasa MUHAS ina programu za masomo 103, kati ya hizo 84 ni za uzamili.

Alisema ukubwa wa matokeo ya utafiti za MUHAS umekuwa ukiongezeka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kufuatana na kiasi cha mikakati na rasilimali zilizowekezwa katika utafiti.

## EPZA: Serikali imeondoa vikwazo kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), imesema serikali imeondoa vikwazo na kero mbalimbali vilivyokuwa vinasababisha wawekezaji kushindwa kuja nchini na wengine kukimbia, hali ambayo imeongeza kwa kiasi kikubwa uwekezaji nchini.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Ntembe, katika kwenye Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Sabasaba yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini, serikali imeendelea kushughulikia vikwazo hasa kwenye maeneo ya sera na sheria ambazo zimekuwa zikiwakwaza wawekezaji na kurudisha nyuma juhudi ya kuvutia wawekezaji wengi zaidi nchini," alisema.

Itembe alisema serikali imetoa baadhi ya vikwazo ikiwamo nafuu ya tozo kurahisishia mwekezaji wa ndani na nje ili naye avutike kuja kuwekeza kwa kuwa kupitia kufanya hivyo kunaleta tija kiuchumi kwa nchi.

Alisema EPZA inatoa vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi katika kuvutia wawekezaji nchini.

"Tunawahimiza watu wenye nia ya kuwekeza katika maeneo mbalimbali nchini watembelee banda letu la Sabasaba la EPZA waweze kupata maelezo zaidi juu ya fursa za uwekezaji zilizopo kwenye sekta mbalimbali ikiwamo kilimo," alisema.

Mfano upatikanaji wa vibali kwa sasa kwa ajili ya wawekezaji imekuwa rahisi na hasa baada ya hivi majuzi kuzindua mfumo maalum unaoitwa 'Business Facilitation Portal' ambao unaweza kujisajili popote duniani kwa ajili ya kuwekeza Tanzania.

"EPZA tunatoa leseni kwa wawekezaji wa ndani na nje na tunaangalia na kutumia busara kwa mwekezaji anayeanza kumtoza gharama kubwa kwani tunatambua mwekezaji anayeanza anahitaji mtaji hivyo lazima tuangalie na kukaa naye mezani kuzungumza naye kisha atoe gharama ambayo haitamsababishia kufilisika na kukimbia," alisema Ntembe.

Alisema, EPZA wamekuwa na jukumu la kusimamia kampuni zinazokuja kuwekeza kwa kuwaonyesha fursa zilozopo katika sekta mbalimbali ikiwamo katika madini, kilimo hivyo wale wote wanaohitaji kuwekeza wanaalikwa kupitia Mfumo wa EPZA kujihudumia popote walipo.

Naye Mkurugenzi wa Uwezeshaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, amesema kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuvutia uwekezaji nchini kutokana na juhudi inayofanywa na serikali kuweka mazingira wezeshi.

"Idadi ya wawekezaji wa ndani na nje imeongezeka sana hasa katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita chini Rais Samia kutokana na juhudi za kupambana na kuviondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji nchini," alisisitiza.

Alisema kwa mfano serikali imeongeza midahalo na wafanyabiashara ili kusikiliza na kupokea kero mbalimbali zinazowakabili hali ambayo imeongeza ufanisi katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Naye Meneja wa uwekezaji uhamasishaji, Panduka Yonaz, alisema kuwa ushiriki wa EPZA katika maonesho ya kimataifa ya Sabasaba yamekuwa fursa muhimu kutoa elimu kwa watu juu ya fursa za uwekezaji nchini na urahisi wa mazingira ya uwekezaji uliowekwa na serikali.

Nakadongo Fares, Ofisa Mkuu wa Uwekezaji Uhamasisha alisema Mamlaka ya EPZA inatoa leseni kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo na hasa uongezaji thamani bidhaa za kilimo kwa ajili ya mauzo nje ya nchi.

# Samia aonya Afrika si kichaka cha rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RIS Samia Suluhu Hassan amesema dunia ijue kuwa Afrika si salama kwa wala rushwa na si kichaka cha ufichaji wa fedha zinazotokana rushwa hiyo.

Aidha, ametaja makundi na taasisi sita kuwa vinara wa rushwa nchini, hivyo kuwaagiza kuchukua hatua na kujirekebisha kwa maendeleo ya taifa. Makundi hayo ni ya wanasiasa, wafanyabiashara, Jeshi la Polisi, Mahakama, taasisi za elimu ya juu na ofisini.

Pia amesema Tanzania imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 139 za matumizi yasiyostahili katika kipindi cha mwaka 2019/20 hadi 2021/22.

Rais Samia, alisema hayo jana wakati akifunga mkutano wa maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Rushwa barani Afrika ulioenda sambamba na maadhimisho ya miaka 20 ya utekelezaji wa mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (AUCPCC) uliotiwa saini mwaka 2003.

"Hapa nataka kusema nchi zetu si kichaka cha kuficha fedha za wala rushwa na si salama kwa wala rushwa na nataka wala rushwa wajue kuwa hatua zaidi zichukuliwe kwa vitendo kwa wale wote wanaohusika na rushwa," alisema.

Alisisitiza viongozi wa Afrika kungana katika mapambano dhidi ya rushwa, lakini kuhusu makundi vinara wa rushwa wakiwamo wanasiasa, aliisisitiza wapewe mafunzo ya masuala ya rushwa.

"Pia naagiza wanasiasa wapelekwe Hong Kong na Singapore kujifunza sababu wamewezaje kukabiliana na rushwa katika nchi hizo ili watumishi wengine hawa katika makundi haya sita vinara wa rushwa nao waende wakajifunza zaidi," alisema.

Alisema wale wote waliotajwa kukithiri kwa masuala ya rushwa wakiwamo wanasiasa, wafanyabiashara, vyombo vya ulinzi na usalama, mahakamani na vyuo vya elimu ya juu zimetajwa kuhusika na masuala ya rushwa hivyo watafuatiliwa kwa ukaribu.

Kuhusu uokoaji wa zaidi ya Sh. bilioni 139 katika matumizi yasiostahili, Rais Samia alisema bado jitihada zinahitajika kukabiliana na janga la rushwa.

"Licha ya kuokoa kiasi hiki cha fedha Tanzania tumeanzisha divisheni ya watuhumiwa wenye mashtaka ya rushwa kubwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, lakini tumeongeza uwazi katika fedha za umma kwa kuanzisha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma mbalimbali, zikiwamo zabuni," alisema. Kadhalika, alisema Tanzania imefanya vizuri katika masuala ya rushwa barani Afrika, huku nchi za Hong Kong na Singapore zikiwa zimefanya vema zaidi kwenye mapambano hayo na kusisitiza wataalamu wa masuala ya rushwa nchini Tanzania kwenda kujifunza zaidi mapambano hayo.

Alitoa ahadi kwa Bodi ya Ushauri ya Mapambano dhidi ya Rushwa barani Afrika (AUABC) kuwa serikali inaendelea na jitihada za kipekee za kutoa jengo la taasisi hiyo badala ya kuendelea kuwepo ndani ya Kituo cha Mikutano ya Kimataifa (AICC).



Pia alitoa rai kwa vyombo vyote ikiwamo vya habari kuzuia na kupambana na rushwa, ili kufikia malengo ya kudhibiti rushwa barani Afrika.

Alisisitiza kuwa Tanzania inakauli mbiu ya "Kuzuia Rushwa ni Jukumu lako na langu, tutimize wajibu wetu" ambayo ni nzito, lakini ni vema ikazingatiwa na kutimizwa na kila mmoja.

Alisema serikali imeanzisha na kusimamia taasisi za kusimamia haki za binadamu, kitengo cha intelijensia lakini serikali itaendelea kufanya vema na kuongeza uwazi katika mapambano dhidi ya rushwa, ikiwamo kuongeza matumizi ya teknolojia ikiwamo matumizi ya TEHAMA.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kamishna Salum Hamduni, alisema maadhimisho hayo yalitanguliwa na matembezi ya amani ya kupinga vita rushwa barani Afrika sambamba na maonesho kutoka TAKUKURU, Taasisi ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) TAKUKURU, Mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na banda maalum la utoaji elimu ya dhana ya rushwa na uhujumu uchumi, taarifa za malalamiko, huduma za utalii na dawa za kulevya.

Kesho (leo) kutafanyika Mkutano wa Wakuu wa Taasisi za Rushwa Afrika ambao utashirikisha washiriki kutoka nchi mbalimbali za Kenya, Burundi, Uganda, Afrika Kusini na nchi nyinginezo ikiwamo mwenyeji Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECCA), Ally Abdallah Ally, alimshukuru Rais Hussein Ali Mwinyi kwa kuleta mabadiliko ya kupambana na masuala ya rushwa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa Barani Afrika (AUABC), Pascoal Joaqium, alisema chombo hiki kimewekwa kama mfumo wa kudhibiti masuala ya rushwa na azimio lilitolewa na wakuu wa nchi katika mapambano ya rushwa barani Afrika.

Pia mikakati mbalimbali itasaidia ufanyaji kazi kwa ufanisi kwa taasisi zinazopambana na rushwa, ikiwamo kutafuta suluhu ya kudumu ya kudhibiti rushwa ikiwamo kuainisha njia za kukabiliana na changamoto za rushwa, ili kufikia ajenda ya malengo ya mwaka 2003.

Alisisitiza taasisi mbalimbali za kupambana na rushwa zimeanzisha mifumo ya kuelimisha wananchi juu ya masuala ya rushwa, ikiwamo kusimamia sheria mbalimbali sanjari na utawala bora katika mapambano ya changamoto za rushwa.

# Utafiti wabaini wananchi wengi kuridhishwa huduma mahakama

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti, Sera na Uchumi (REPOA), Dk. Donald Mmari, amesema asilimia 88 ya wananchi walioshiriki utafiti wa kuangalia utoaji huduma za mahakama, wameelezea kuridhishwa nazo na kuna mabadiliko makubwa.

Dk. Mmari alisema hayo jana katika Kituo Jumuishi Temeke wakati wa kukabidhi ripoti kuhusu kuridhishwa kwa watumiaji wa huduma za mahakama kwa mwaka 2023.

Alisema REPOA ilianza kufanya utafiti katika mahakama mwaka 2015 na 2019 na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha na kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2023 maboresho makubwa yamefanyika.

Akisoma ripoti hiyo, Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo wa REPOA, Dk. Lucas Katera, alisema wameangalia maeneo mengi, ikiwamo wananchi wanajisikiaje wanapofika mahakamani.

"Hapo wananchi kwa asilimia 90 wanaamini wakifika mahakamani watatoka salama, kama amekosa atahukumiwa na kama si mkosaji ataachiwa.

"Wananchi watumiaji huduma za mahakama kwa asilimia 88 mwaka 2023 wanaridhishwa na huduma zinazotolewa. Idadi ni kubwa kulinganisha na mwaka 2019 walioridhishwa walikuwa asilimia 78," alisema.

Alisema kwa mahakama zote, wananchi wanaridhishwa na huduma kwa asilimia 90, wasioridhishwa hawazidi asilimia tano lakini Mahakama ya Kazi wasioridhishwa na huduma ni asilimia 23.

Akizungumzia maadili, alisema imeonekana kwamba katika mahakama za chini asilimia 25 waliitoa zawadi ili kazi zao zifanyike kwa haraka."Wananchi hawatumii tovuti ya mahakama kuangalia vitu mbalimbali wakidai hawana taarifa, tumetoa mapendekezo kwa ajili ya maboresho," alisema.

Aliyataja maboresho yanayotakiwa kufanyika kuwa ni kuongeza maeneo ya kutoa huduma za mahakama, muda wa kesi kuanza na kumalizika uzingatiwe, ukaguzi ufanyike katika mahakama na itolewe elimu, ili wananchi wajue huduma zinazotolewa na mahakama kwa mtandao.

Akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma, alisema matokeo yanaonesha kiwango cha umma kuridhishwa na huduma za mahakama ni kikubwa.

Alisema baada ya kufanya maboresho yaliyopendekezwa katika ripoti ya mwaka 2015 ambayo kiwango cha kuridhika kilikuwa asilimia 61 na ripoti ya mwaka 2019 ambayo kiwango kilikuwa asilimia 78, mwaka 2023 kiwango kiliongezeka na kufikia asilimia 88.

"Maboresho mengi ya huduma za mahakama kwa ripoti zilizopo yamefanyika kama vile matumizi ya TEHAMA, uendeshaji wa mashauri kwa njia ya kielektroniki, kuanzishwa kwa mahakama inayotembea (mobile court)," alifafanua.

Alisema hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwamo ujenzi wa vituo jumuishi sita vya utoaji haki, kujenga mahakama mpya za wilaya na mwanzo, kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

Pia kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja, kutoa elimu kwa umma, kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa huduma za mahakama kwa asilimia 98, kutoa nakala za hukumu bure, kupunguza mrundikano wa mashauri kutoka asilimia 11 hadi 4 na kuajiri watumishi wapya.

"Maeneo yaliyopendekezwa kufanyiwa maboresho kutokana na ripoti ya mwaka 2023 ni elimu kwa umma na muda wa usikilizaji mashauri mahakama inaendelea kuyafanyia kazi.

"Kutokana na maoni ya wananchi katika maeneo ya kuboresha, tutaendelea kuyafanyia kazi ili kuboresha zaidi," alisema Msajili Mkuu.

"Tuko katika hatua za mwisho katika mfumo ulioboreshwa wa usimamizi wa mashauri, mfumo unaoipeleka Mahakama katika matumizi yasiyotumia karatasi," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa wananchi kuwa na imani na Mahakama ya Tanzania na kutoa ushirikiano, ili kuiwezesha mahakama kutoa haki.

## UFAFANUZI

Katika toleo letu Na. 0581358 la Jumamosi tarehe 1 Julai 2023, Ukurasa wa Tano (5), tulikuwa na tangazo la hesabu za mwisho za Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

Hata hivyo, katika tangazo hilo, kulikuwa na kosa la kichwa cha habari cha tangazo hilo kusomeka

'THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA MUNICIPAL COUNCIL

THE REPORT BY THOSE CHARGED WIT GOVERNANCE AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2022'.

badala ya kusomeka

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA DISTRICT COUNCIL

THE REPORT BY THOSE CHARGED WIT GOVERNANCE AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2022

Hivyo, maneno sahihi katika kichwa cha habari cha tangazo la hesabu za halmashauri hiyo yanapaswa kusomeka 'Kyela District Council' badala ya 'Kyela Municipal Council' iliyosomeka awali.

Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Mhariri

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mafunzo ya JKT kwa vijana huwajengea ukakamavu, kujitegemea na nidhamu

**MIAKA** ya nyuma wakati mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa vijana wanaomaliza elimu ya kidato cha sita kuwa ni lazima, yalisaidia kuwakutanisha, kuwajengea mshikamano na elimu ya kujitegemea.

Walikuwa wakitoka kwenye mafunzo hayo wanakuwa na nidhamu ya hali ya juu ya jinsi ya kujitegemea na vile vile yalisaidia kukutanisha vijana kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania na kuwa kitu kimoja.

Vijana pia walikuwa wakakamavu na walikuwa na uwezo wa kujiajiri badala ya kutegemea ajira za kuajiriwa.

Kutokana na umuhimu wa mafunzo hayo, serikali imeona kuna haja ya kuunganisha Mpango wa Jenga Kesho iliyobora kwa Vijana (BBT) kwenye kambi za mafunzo ya JKT ili kuongeza fursa za vijana kujitegemea na kushiriki shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

Katika maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa JKT yaliyofanyika juzi, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema lengo ni kuwawezesha vijana hao pindi watakapohitimu mafunzo kupata fursa ya kushiriki shughuli hizo.

Serikali imedhamiria kuiwezesha JKT kuwa ya kisasa zaidi yenye kuendana na mahitaji ya sasa katika kutimiza majukumu ya malezi ya vijana kuwajenga uzalendo wenye kulithamini taifa, kujitegemea uzalishaji mali na kulitetea taifa bila hofu.

JKT inawafunza vijana kuingia katika maeneo mengine ya kazi kwa kujitegemea ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Mpango wa taifa wa miaka mitano unahimiza uwezeshaji vijana ambao umegawanyika katika maeneo mbalimbali likiwamo kuwawezesha vijana kufunguka kiuchumi.

JKT imekuwa ikitengeneza ajira jambo ambalo limesisitizwa kwenye mpango huo wa maendeleo wa miaka mitano, lengo ni kuwawezesha vijana kupunguza utegemezi ili nchi iweze kujiendesha, serikali inakuja na programu nyingi za kuwawezesha vijana na kwa sasa programu maarufu ni Kujenga Kesho iliyobora kwa Vijana inayowapeleka vijana kwenye masuala ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Pia dhamira ya serikali ni kuiwezesha SUMA JKT kupata mikopo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na endapo kama kukihitajika udhamini, serikali ipo tayari.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, anasema mafunzo ya JKT ni muhimu na yana mchango wa amani iliyopo nchini na wataendelea kushirikiana na wizara za kisekta kuboresha mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana wa jeshi hilo ili kupata stadi na maarifa tofauti na ilivyo sasa.

Baada ya mafunzo, vijana watakuwa na uwezo wa kujitegemea na kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasiriamali, maendeleo ya michezo na sanaa.

Rais ameongeza bajeti kwa JKT na kuwezesha kuongeza idadi ya kuchukua wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita kujiunga na JKT kwa lazima kutoka 30,000 hadi 52,000.

Katika kuhakikisha JKT inajitegemea kwa chakula na kuchangia usalama kwa chakula nchini, JKT inatekeleza mradi wa skimu ya umwagiliaji ambayo iko katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Katika kipindi chote, JKT imejihusisha na uzalishaji mali kupitia vikosi na Shirika la Uzalishaji Mali (SUMA JKT) katika sekta za ujenzi, kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara hivyo kuchangia gharama za mafunzo ya vijana na kutoa gawio serikalini, kulipa kodi na kuongeza ajira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Maelekezo ya CCM yamalize mjadala

**KUMEKUWAPO** na mjadala unaoendelea katika mitandao ya kijamii, kwenye mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na hata miongoni wa watu kwenye vyombo vya usafiri kuhusu bandari.

Ni hatua ya serikali kuingia makubaliano na ukodishaji wa bandari ya Dar es Salaam na kampuni ya kimataifa ya DP World ya Dubai.

Watu wamekuwa wakihoji mazingira ya mkataba huo pamoja na vipengele vilivyomo, huku baadhi wakionya kuhusu hali hiyo na kutaka ufafanuzi zaidi kuhusu uwekezaji huo.

Mjadala huo umeyavutia makundi ya aina mbalimbali kuanzia wanasiasa, wataalamu wa sheria, viongozi wa dini na watu wengine wa kawaida katika jamii, wakiwapo wanaoonyesha ukosaji wa waziwazi.

Wakati mjadala huo ukiendelea, Halmashauri Kuu ya CCM inaingilia kati na kuja na maazimio matatu yanayogusa uwekezaji huo, mojawapo ikiwa ni kuitaka serikali kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu uhalisia uliomo katika makubaliano ya uwekezaji huo.

Kwa mujibu wa Katibu wa Halmashauri Mkuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema anasema halmashauri hiyo imeazimia kuwa uwekezaji na uendeshaji wa bandari ni kwa manufaa ya uchumi wa nchi. Lakini, pia katika azimio la tatu, anasema halmashauri imekubaliana kuwa uwekezaji huo ni utekelezaji wa vitendo wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025, ibara ya 59, ukurasa wa 92.

Uamuzi wa CCM wa kutaka serikali iongeze kasi ya utoaji wa elimu juu ya sakata hilo la uwekezaji, ni ni jambo la muhimu, hasa kutokana na ukweli kwamba kila mmoja amekuwa na lake la kusema na kuwafanya wananchi washindwe kuelewa ni nani yuko sahihi.

Kwa kuzingatia ukubwa wa jambo lenyewe, ni wazi wananchi wakielimishwa, wanaweza kuelewa, kwani kumekuwapo na taarifa nyingi zenye mkanganyiko ambazo zinahitaji kufafanuliwa.

Ingawa kumekuwapo na majadiliano ya wazi kupitia mtandao wa club house, kwa ajili ya kulijadili suala hilo hilo, lakini hatua iliyochukuliwa na CCM ya kutaka kasi ya utoaji wa elimu ni nzuri zaidi.

Kama inawezekana, basi serikali isambaze watumishi wake nchi nzima kutoa elimu hiyo ili iwe rahisi kwa wananchi wa kawaida kuelewa ni nini kinaendelea katika nchi yao.

Ikumbukwe kuwa vyama vya siasa navyo vinaendelea na mikutano ya hadhara katika maeneo mbalimbali nchini, moja ya ajenda za mikutano hiyo ni kuhusu uwekezaji kwenye bandari ya Dar es Salaam.

Kupitia elimu itakayotolewa, wananchi wataelewa ukweli uko wapi, ili kuondoa sintofahamu inayoendelea mitandaoni, vijiweni na katika mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Hatua ya CCM kuagiza serikali kuongeza kasi ya utoaji wa elimu, ni wazi kwamba kasi ya sasa ni ndogo kuliko ya makundi mengine yanayojadili uwekezaji huo na kuuchambua.

Ni wakati sasa kwa waliopewa jukumu hilo kujipanga na kwenda kusambaza elimu, ili hatimaye Watanzania wapate mwanga na kumaliza sintofahamu ambayo inaendelea sasa.

Kumekuwapo na maneno yanayotumika kama kuuzwa, kubinafsisha na kukodishwa bandari. Hayo yote yanahitaji ufafanuzi wa kina na inawezekana ndiyo maana CCM ikaeleza utoaji wa elimu.

Badala ya Watanzania kuendelea katika giza la kutofahamu kile ambacho serikali inakusudia kukifanya. Ni wazi kupitia elimu ambayo itatolewa, inaweza kuwa rahisi kila kitu kujulikana.

Kwa ujumla, mengi yamesemwa kuhusu uwekezaji huo, ikiwamo malalamiko huku wengine wakitaka kuukwamisha na baadhi wakitaka uwepo. Lakini njia bora ya kuweka mambo sawa inaweza kuwa hiyo iliyoelekezwa na chama tawala kwa serikali.

Pamoja na hayo, mjadala huo usiwe chanzo cha kuwagawa Watanzania kwa misingi ya itikadi za vyama, ukabila au udini, bali ungezingatia umoja wa kitaifa kwa masilahi ya nchi.

Ikumbukwe bandari hiyo ni muhimu kwa Tanzania na na mataifa jirani ya Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, yanayoitegemea pia.

Lakini kumekuwapo na sintofahamu ya utendaji kwenye bandari hiyo na kusababisha serikali kuwaondoa wakurugenzi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ubadhirifu wa fedha.

Kwa Mujibu wa Msemaji wa Serikali, Grayson Msigwa, serikali inaona kuna haja ya kumpa bandari hiyo mwekezaji ili kuongeza ufanisi na mapato.

# Bandari Tanga yapata ongezeko shehena ya mizigo

**Na Mwandishi Wetu**

TAKWIMU za ongezeko la shehena za mizigo katika Bandari ya Tanga kwenda maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi zimeripotiwa kuongezeka kwa asilimia 8.2 ikiwa ni ongezeko ndani ya miezi sita kwa mwaka 2023.

Akizungumza wakati akifungua Mkutano wa Kamati ya Maboresho ya Huduma za Bandari kwa Bandari ya Tanga mkoani humo, Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi-Sekta ya Uchukuzi, Mhandisi Aron Kisaka, amesema serikali inategemea ongezeko zaidi baada ya maboresho yaliyofanyika na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inapashwa kuhakikisha kitengo cha masoko kinajipanga.

"Baada ya uwekezaji kwenye miundombinu hususani gati na vitendea kazi tutegemee mzigo mwingi zaidi hivyo ni wajibu wa idara ya masoko kuhakikisha mzigo unahudumiwa vizuri ili kufanya wateja wasihame Bandari ya Tanga," alisema Mhandisi Kisaka.

Aliitaka TPA kuhakikisha inaongeza kasi kwenye mazungumzo na kampuni nyingine ya meli ili idadi ya mzigo iongezeke na hatimaye uwekezaji kuwa na tija kwa serikali na jamii kwa ujumla.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Peter Milanzi, alisema serikali kupitia TPA kwa mwaka 2023/24 imejipanga kuongeza gati mpya mbili kwa kutenganisha abiria na mizigo ili kurahisisha shughuli za uchukuzi katika bandari hiyo.

Naye mdau wa bandari nchini, Lilian Mbwambo kutoka Kampuni ya Uwakala wa Meli ya Tanga Modern, alisema utaratibu wa serikali wa kuwa na vikao vya pamoja na wadau wote kutarahisha kutatua changamoto zilizopo kwa wakati ili kurahisisha usafirishaji katika bandari hiyo.

Serikali kupitia TPA imekuwa ikiendesha vinavyowakutanisha wadau wote wanaoshughulikia na bandari kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za uendeshaji kwa pamoja.






Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi-Sekta ya Uchukuzi, Mhandisi Aron Kisaka, akisisitiza jambo kwa wadau mbalimbali wa huduma za bandari nchini (hawapo pichani), alipofungua mkutano wa kamati ya maboresho ya huduma za Bandari ya Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika la Madaktari Afrika latoa msaada vifaa tiba bil. 1/-

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Madaktari Afrika lililopo nchini Marekani limetoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni moja ambavyo vitatumika katika kambi maalumu ya siku tano ya matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo.

Kambi hiyo iliyoanza leo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), imelenga kubadilishana uzoefu baina ya wataalamu wa afya wa JKCI na wenzao kutoka Shirika la Madaktari Afrika, kuwasaidia wagonjwa vifaa vya matibabu hayo na kutoa huduma ya mfumo wa umeme wa moyo.

Akizungumza na madaktari wanaotoa matibabu katika kambi hiyo alipowatembelea jana jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, aliwashukuru Madaktari Afrika kwa msaada walioutoa na kusema magonjwa ya mfumo wa umeme wa moyo ni sehemu ngumu kwenye masuala ya tiba ya moyo.

Aliwapongeza madaktari hao kwa kuwa mstari wa mbele kushirikiana na wataalamu wa JKCI kuokoa maisha ya Watanzania.

"Rais wetu alishawekeza mtambo wa kisasa wa kutibu umeme wa moyo, upande wa suala la tiba tumejitahidi kupata wataalamu wenye uwezo wa kutoa huduma bora kuendana na teknolojia iliyopo, hatuna budi kushirikiana nanyi kwani muda mrefu mmekuwa mkitoa matibabu haya," alisema Dk. Mollel.

Dk. Mollel alisema mbali na kubadilishana uzoefu madaktari hao wanajua kwamba kuna Watanzania wenye matatizo ya umeme wa moyo, lakini hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu na kuleta vifaa vya matibabu kuwatibu wasiokuwa na uwezo wa kugharamia.

"Kupitia kambi hii wataalamu wetu wataenda kubadilishana uzoefu na kuendeleza teknolojia katika kutoa huduma za matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo na kuifanya taasisi hii kutambulika katika nchi nyingi zilizotuzunguka hivyo badala ya kuwapeleka wagonjwa wao barani Ulaya sasa wanasaini mikataba na JKCI ili wagonjwa wao watibiwe hapa nchini kutokana na uwezo wetu kupanda hadi kufikia asilimia 97," alisema Dk. Mollel.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, alisema madaktari kutoka Shirika la Madaktari Afrika wamekuja na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni moja ili kuwasaidia wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kugharamia matibabu hayo.

"Madaktari Afrika ni marafiki zetu ambao wanashirikiana nasi kwa muda mrefu, wamefika hapa kwaajili ya kuwafundisha madaktari wetu na kuwasaidia wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo kutokufanya kazi vizuri," alisema Dk. Kisenge.

Dk. Kisenge alisema katika kambi hiyo wagonjwa wenye matatizo makubwa ya mfumo wa umeme wa moyo watapatiwa matibabu na mabingwa hao wakiwa na lengo la kutoa huduma za matibabu pamoja na kubadilishana uzoefu na madaktari, wauguzi na wataalamu wa kuendesha mtambo wa Cathlab.

Naye Daktari bingwa wa mfumo wa umeme wa moyo kutoka Shirika la Madaktari Afrika David Singh, alisema katika kambi hiyo wanashirikiana na madaktari wa JKCI kujifunza mbinu mpya za matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo ili kuendana na maendeleo ya teknolojia ya matibabu.

"Tumefika katika taasisi hii kwasababu tuna taarifa za huduma bora zinazotolewa kwa wagonjwa wanaotibiwa hapa, hivyo tukaona ni sehemu sahihi ambayo tunaweza kushirikiana na kuboresha huduma zaidi," alisema Dk. Singh.

Aidha, alisema Shirika la Madaktari Afrika litaendelea kushirikiana na wataalamu wa Afya wa JKCI kwani kwa sasa taasisi hiyo inafanya vizuri katika utoaji wa uchunguzi na matibabu ya moyo Afrika Mashariki na kati.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wananchi watakiwa kujenga tabia kuvuna maji ya mvua

Na Elizabeth Zaya

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imewataka wananchi kujenga tabia ya kuvuna maji ya mvua kwa mifumo inayofungwa majumbani na katika taasisi zao ili kuwa na akiba ya kutosha na kukabialiana na upungufu wa maji hayo ambao hujitokeza kwa baadhi ya misimu.

Kauli hiyo ilitolewa na Mhandisi Mwandamizi wa Maji wa EWURA Kanda ya Mashariki, Amani Nyekele, katika banda lao la maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF).

Alisema uvunaji wa maji ya mvua ni teknolojia inayokusanya na kuhifadhi maji ya mvua kutoka juu ya paa, ardhi na kwenye miamba kwa kutumia mbinu na vifaa mbalimbali ikiwamo mitungi, tangi, bwawa na kwamba kazi hiyo inahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali katika kutatua tatizo la upungufu wa maji.

Pia alisema yapo mambo mengi ya kuzingatia wakati wa uvunaji wa maji ikiwamo kuhakikisha vyombo vinavyotumika kwa kazi hiyo vinakuwa ni safi kwa ustawi wa afya ya watumiaji.

"Na tunashauri kwamba kabla ya kuanza kuvuna maji, ni lazima vyombo vinavyotumika kuvunia maji hayo vioshwe kwanza kwa kutumia dawa maalumu ili kuua vijidudu ambavyo vinaweza kuwapo kwenye maji na tunashauri kwamba baada ya maji kuvunwa ni vyema kuyachunguza mara kwa mara na kuweka dawa ili yaendelee kufaa kwa ajili ya matumizi," alisema Nyekele.

**Alisema ni vyema kila mtu kuwa na mipango mizuri na sahihi ya matumizi ya maji kuendana na hali ya upatikanaji wa maji hayo katika eneo alilopo.**

"Bado hatujapata mahali ambapo wananchi wanasema wanajitosheleza asilimia zote katika upatikanaji wa huduma ya maji, kwa hiyo tunaendelea kuelimisha umma kutumia njia mbadala kuhakikisha watu wanavuna maji ya mvua ambayo ni rahisi kuyavuna kuliko yale yanayotoka ardhini au kwenye mabwawa ambayo yanahitaji kuyasafisha."

Alisema, wataendelea kutoa elimu ya kiufundi kwa wananchi namna ya kuvuna maji hayo na njia rahisi ni kutumia paa iliyo tayari.

Alisema ni vyema kila mtu kuwa na mipango mizuri na sahihi ya matumizi ya maji kuendana na hali ya upatikanaji wa maji hayo katika eneo alilopo.

"Kwa mfano kuna baadhi ya maeneo yenye ukame, watu wa maeneo haya ni lazima wawe makini sana katika matumizi bora ya maji, lakini kuhakikisha hawapitwi na misimu ya uvunaji wa maji ya mvua," alisema Nyekele.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (fulana ya bluu), akiwa na Katibu Mkuu wa Chama cha RPF cha Rwanda, Wellars Gasamagera (katikati) na wageni wengine wakimsikiliza Meneja wa Wakala wa Vipimo, Temeke, Krishna Mahamba, kwenye Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Halotel yaboresha huduma kuwafikia wateja wengi zaidi

Na Zuwena Shame

KAMPUNI ya Halotel imedhamiria kufanya maboresho katika kupanua wigo kwa wateja wake kwa kubadili logo ili kuendana na huduma stahiki.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Biashara wa kampuni hiyo, Abdallah Salumu, wakati wa maonyesho ya kimataifa ya biashara ya 47 yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa kubadilika kwa logo ya Halotel ni moja ya maboresho ya kampuni hiyo kwenye huduma zake mbalimbali, ikiwamo huduma za intaneti kwenda 4G nchi nzima. Salumu alisema katika msimu huu wa maonyesho ya Sabasaba pia wanaendelea kutoa 'offer' mbalimbali kwa wateja wao wa awali na wapya watakaojisajili na mtandao wa Halotel na wale wanaobadili laini zao kwenda 4G.

"Moja ya maboresho yetu kwa sasa ni kubadilisha logo yetu na kuwa na mwonekano unaoendana na huduma zetu mpya zilizoboreshwa zaidi. Wateja wetu sasa wataweza kupata huduma zetu za 4G za intaneti bila vikwazo," alisema Salumu.

Alisema baadhi ya offer ambazo Halotel wanaendelea kutoa kwa wateja wake wapya na wanaobadilisha laini zao za simu kwenda 4G katika msimu huu wa sikukuu ya Sabasaba ni pamoja na muda wa maongezi, t-shirts, vikombe, keyholder na kofia.

# Muliro ataka polisi kutenda haki wanapopokea malalamiko

Na Maulid Mmbaga

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amebainisha kuwapo watu wanaodanganya kuhusu madai, malalamiko na kesi mbalimbali.

Alisema ni vizuri askari kutoamini yeyote na badala yake wanapoletewa malalamiko wachunguze kwa usawa kabla ya kuchukua hatua.

Muliro aliyasema hayo jana akiwa kwenye banda la jeshi hilo katika maonesho ya Sabasaba akieleza kuwa ili wananchi waache kuwachukia ni muhimu askari polisi kufanya uchunguzi wa haki na usawa wanapopelekewa malalamiko yoyote.

"Kwa mfano mimi nimeshatuhumiwa, lakini najijua sijafanya hilo tendo, mwokozi wangu ni polisi, wewe umeshaniripoti, polisi akiamini asilimia 100 akaacha kuchunguza kwa sababu wewe umeripoti akaanza kunipokea kama mtuhumiwa kwa makofi haitakuwa sawa," alisema na kuongeza;

"Akinitreat (akinichukulia) kama mhalifu bila kuchunguza akategemea ushahidi wako ambao unaweza kuwa wa ukweli au uongo, ndivyo walivyo polisi wengi, wanaamini ushahidi kutoka kwa mlalamikaji kuliko mtu anayetuhumiwa, sasa tunapokosa fair investigation (uchunguzi wa haki), tunajenga wimbi kubwa la watu kulichukia jeshi," alisema Muliro.

Pia alisisitiza askari polisi ni lazima wafanye uchunguzi ambao hauleti mashaka wanapoletewa malalamiko yoyote, akishauri pia kutumika kwa uchunguzi wa kisayansi.

"Kuna msemo unasema sasa sayansi haiongopi, umefanya! Umefanya, hukufanya! Hukufanya, muwaamini wote kwa asilimia 50 kila anayeletwa usiseme amefanya, sio kila anayeletwa ni mhalifu waongo ni wengi," alisema Muliro.

Hata hiyo, aliwasisitiza askari polisi kwamba wanatakiwa kuwa makini na watulivu na kwamba wanapoletewa jambo lolote hata likiwa kubwa kiasi gani liwe na uchunguzi wa 50 kwa 50, akieleza kuwa wanaweza kuletewa uongo mkubwa, lakini jukumu lao ni kuchunguza.



"Ukilichukua kama lilivyo tunazidi kuongeza mianya ya watu kulichukia jeshi na askari kwasababu mimi najua niko 'innocent' (sina hatia) anayetakiwa aniokoe ni polisi sasa anashindwa kuniokoa anaenda kuokolewa na mahakama lazima nitaishukuru kwasababu ndiyo imenigundua wema wangu," alisema Muliro.



## HABARI KASKAZINI

# Msigwa atembelea eneo ujenzi ukumbi mikutano

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Greyson Msigwa, ametembelea eneo lenye ekari 21 ambalo litajengwa Kituo kikubwa cha Mount Kilimanjaro, chenye ukumbi mkubwa wenye uwezo wakuchukua watu 3,000 ili kuleta mapinduzi ya utalii wa mikutano barani Afrika.

Aidha katika kituo hicho, kutajengwa eneo la maonyesho litakalokuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 1,000, hoteli yenye hadhi ya nyota tano itakayochukua watu zaidi ya 1000, maduka makubwa yatatoa fursa kwa wafanyabiashara kuhudumia watalii watakaofika nchini.

Akizungumza jana jijini Arusha baada ya kutembelea eneo hilo lililoko Kijenge, Msigwa amekipongeza Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC) kwa mawazo yatakayoleta mapinduzi makubwa katika utalii wa mikutano ya kimataifa nchini na Afrika.

"Serikali inatazama Arusha kama Mkoa wa kimkakati katika sekta ya utalii, hivyo tunahitaji kuongeza bidhaa ya utalii ya mikutano mikubwa kuja hapa na tukifanikiwa ujenzi huu tutaongeza idadi ya watilii kuja katika hifadhi zetu na lengo letu la ifikapo mwaka 2025 kufikia watalii milioni tano, tutalifikia na mapato yataongezeka zaidi," alisema.

Msigwa, alisema pamoja na UVIKO-19 kuiyumbisha Tanzania, lakini kwa sasa imepiga hatua zaidi ambapo kwa mwaka jana 2022 imepokea watalii zaidi ya milioni 1.4 ila lengo ifikapo mwakani wafike watalii zaidi ya milioni mbili na inawezekana.

"Watalii wakifika nchini na kupata huduma bora lazima taarifa zitasambaa na idadi yao itaongezeka, tunataka watalii wakifika katika mkutano, wapate sehemu ya kulala nzuri inayoambatana na huduma bora za kisasa na kwenda hifadhini," alisema.

Kadhalika, alisema mafanikio yoyote ya kiuchumi yakitakiwa lazima kushirikiana na sekta binafsi, hivyo vizuri Watanzania wakaielewa serikali pale inapohitaji kushirikisha wawekezaji kuwa wana dhamira njema.

Alikipongeza Kituo cha AICC kwa mwaka jana pekee, kimeliingizia taifa mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 17, lakini ujenzi wa kituo hicho cha Mount Kilimanjaro kikikamilika, watafikia ukusanyaji wa mapato zaidi ya Sh.bilioni 50 hadi 100 kwa mwaka.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa AICC, Balozi Ephraim Mafuru, alisema uamuzi wa kudhamiria kujenga kituo hicho kikubwa, umekuja baada ya kuona kwa miaka 45 tangu kuanzishwa kwa AICC hakijaweza kukidhi mahitaji ya sasa ya soko la utalii wa mikutano duniani.

"Licha ya kuwa na kituo kingine cha mikutano ya kimataifa kilichopo jijini Dar es Salaam cha Julius Nyerere (JNICC) lakini Arusha kama kitovu cha utalii, serikali imekuja na uamuzi wa kuwekeza zaidi katika eneo hili la ekari 21, ambalo lipo ndani ya ekari 90 za AICC kwa kuamua kubadilisha matumizi ili kuongeza mapato na idadi ya watalii," alisema.

Alisema kwa upande wa hoteli wanatarajia kujenga hoteli mbili za hadhi ya nyota tano, lakini kwa kuanza wataanza na ujenzi wa hoteli moja, ambapo pia wanatarajia eneo hilo kupokea viongozi zaidi ya 15 hadi 20 na kuwahudumia kwa wakati mmoja.

"Tanzania kwa sasa tumepanda hadi nafasi ya tano toka nafasi ya 11 kwenye utalii wa kumbi za mikutano na hoteli, ikitanguliwa na nchi za Afrika Kusini, Morocco, mMisri na Rwanda, ila tukiwekeza zaidi tuna uwezo wa kushika nafasi hata ya tatu," alisema.

# MoCU yapongeza ufadhili kuwezesha ushirika

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Sife, amelishukuru Shirika la We Effect East Afrika na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA), kwa kufadhili mradi wa miaka mitano wa kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika na asasi za kijamii nchini.

Akizungumza jana, wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya uongozi wa mabadiliko yaliyo chini ya mradi huo, Prof. Sife alisema MoCU inawashukuru wafadhili hao kwa kutambua na kuwashirikisha katika utekelezaji wa mradi huo, unaolenga kuchangia juhudi za serikali katika kupunguza umaskini nchini.

Awali, Meneja Mradi huo na Mhadhiri Mwandamizi wa MoCU, Dk. Neema Kumburu, alisema mafunzo hayo yanatekelezwa kupitia mradi wa kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii (CACOSMBO).

Alisema mradi huo unaotekelezwa na MoCU unachangia utekelezaji wa mradi mkubwa wa The Livelihood and Right to Food (LRF) ambao malengo yake makubwa ni kuhakikisha kuna kuwa na haki ya chakula kwa wanawake, vijana na watoto katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

"We Effect wanatambua kwamba haki ya chakula inaweza kufikiwa iwapo tu kutakuwa na mifumo yenye usawa katika suala zima la kufikia haki ya chakula na ubora wa maisha kwa mwananchi wa kawaida.

"Tutafanya utafiti na mwisho wa siku tunatarajia kila mwananchi wa Tanzania kwa namna moja au nyingine yeye ni mwanachama wa Chama cha Ushirika wa kifedha, uwe ushirika wa masoko, uwe ushirika wa uvuvi au aina nyingine yeyote ile ya ushirika," alisema.

Meneja wa We Effect Tanzania, Frank Ademba, alisema shirika hilo limewapatia wadau 12 wakiwamo MoCU, zaidi ya Sh. bilioni tisa, kwa ajili ya kuhakikisha wanatekeleza na kufikia matokeo ya mradi yaliyopangwa kwa muda wa miaka mitano, ili jamii yote iweze kunufaika.

Wanufaika wa mradi huo ni vyama vya ushirika, vyama vya wakulima, taasisi za fedha, na wanaofanya kazi ya kuwekeza pesa ndani ya vikundi na kukopeshana kwa ajili ya kuimarika katika mfumo mzima wa kijamii.

Baada ya uzinduzi huo, Prof. Baltazar Namwata wa MoCU, akitoa nasaha zake, alisema licha ya serikali kuwa mdau wa kwanza katika maendeleo, lakini ina jukumu kubwa la kuweka mazingira saidizi ili wadau wengine wote waweze kushiriki kwa namna moja au nyingine kutekeleza mipango ya kitaifa.

"Katika mradi huu serikali ina jukumu kubwa la kuendelea kuvilea vyama vya ushirika na taasisi za kijamii ziweze kutimiza majukumu yake na moja ya changamoto ambazo zinakwamisha hivi vyama vya ushirika na taasisi za kijamii kuweza kutekeleza majukumu yao ni ukosefu wa fedha.

Prof. Namwata aliongeza kuwa: "Tumesukumwa kufanya haya kwa sababu moja ya majukumu ya msingi ya chuo chetu ni kulea na kuvijengea uwezo vyama vya ushirika.

"Kupitia mradi huu, We Effect, imetuongezea wigo wa kufikia wadau wengi ikiwamo vyama vya ushirika na taasisi za kijamii ili kuzijengea uwezo kupitia hii programu ya uongozi, tunaamini tutakuwa na mchango mkubwa sana katika kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika na taasisi za kijamii."

Alex Urio, Mratibu wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Mkoa wa Kilimanjaro (MVIWAKI), ambaye ni mbia wa mradi huo, alisema wanaona ujio wa mradi huo wa kuboresha chakula pamoja na maisha, utakuwa na manufaa makubwa na utaleta matokeo chanya.

"Kwa sababu pamoja na mambo mengine, wenzetu wa We Effect, wamelenga katika kuboresha masuala ya uongozi kwa vikundi na wana ushirika, lakini kuboresha upande wa lishe kwamba mtu anakula nini na anakula ili iweje lakini pia suala zima la uboreshaji na masoko," alisema Urio.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa pili kushoto), akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kushoto), alipotembelea machimbo ya madini ya Tanzanite eneo la kitalu C kinachomilikiwa na Kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd katika mji mdogo wa Mirerani juzi. Wa tatu kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Onesmo Mbise. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shirika lajitosa udhibiti uharibifu mazingira

**Na Mary Mosha,** SIHA

SHIRIKA la Teen Missions International in Tanzania, limejitosa kutafuta ahueni ya uharibifu wa mazingira katika ukanda wa tambarare wa wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, ambao unatishiwa na mabadiliko makubwa ya tabianchi.

Wadau hao wanaotoa huduma za kiroho, wameanza kampeni hiyo kwa kupanda zaidi ya miti 1,000 katika Hospitali ya Wilaya ya Siha ili kukabiliana na mabadiliko hayo na kuandaa mazingira rafiki ya wagonjwa kupumzika wanaposibiri huduma za uchunguzi na matibabu.

Akizungumzia kampeni hiyo jana, Kiongozi wa Shirika hilo, Japhet Mponde, alisema lengo la kuotesha miti hiyo ni kuweka mazingira salama na bora kwa wagonjwa, wakati wanaposubiri huduma za matibabu pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea duniani kote.


"Tumeamua kuotesha miti katika Hospitali ya Wilaya ya Siha ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kutunza mazingira, kuongeza vivuli, hasa ikizingatiwa hospitali kuna kuja watu wa maradhi tofauti tofati na wanahitaji hewa ya kutosha," alisema Mponde.

Aidha, Kiongozi wa Shirika hilo kutoka Marekani, Russell Decker, alisema wamekuja na vijana kutoka nchini Marekani wenye matamanio ya kutunza mazingira na kuhubiri Injili ya Mungu. "Shirika letu lipo katika nchi zaidi 35 duniani na Tanzania ni mojawapo. Tumekuja chini Tanzania na tayari tumeweka alama katika Hospitali ya Wilaya ya Siha. Kupanda kwetu miti 1,000 ni kuionyesha jamii kwamba tunaguswa zaidi na ajenda ya utunzaji wa mazingira, ambayo ni ya kidunia na sio ya watu wache," alisema.

Miti hii ikitunzwa vizuri na ikikua itasaidia kuvuta mvua kwa wakati, kukabiliana na ukame, utunzaji wa theluji katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, upatikanaji wa hewa safi kwa wagonjwa waliolazwa katika hospitali hii au watakaokuja kupata huduma hapa," aliongeza.

Baada ya kupandwa miti hiyo, Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Huduma za Afya wa Wilaya ya Siha, Placidia Josephat, aliwashukuru wadau hao kwa kuendesha kampeni hiyo kila nchi wanayokwenda kutoa huduma za kiroho na kuacha alama katika uhifadhi wa mazingira.

Kwa mujibu wa Josephat, katika wilaya hiyo hasa maeneo ya ukanda wa tambarare, kipindi cha nyuma kulikuwa na tatizo la ukame uliopitiliza, hali ambayo ilisababisha kuwapo makali ya mgao wa maji katika vijiji vingi.





# Wadaiwa kupiga simu zimamoto kutafuta wachumba, freemason

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza limeeleza kero linazokumbana nazo katika utendaji kazi, ikiwamo kupokea simu za watu wasio na shida wakati mwingine wakiulizia kama wanaweza kupata wachumba au kuunganishwa na 'Freemason', hatua ambayo inakwamisha ufanisi wa kudhibiti majanga.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Mrakibu (SF) Kamila Labani, alisema hayo jana baada ya kuwavisha vyeo kwa niaba ya Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji nchini, John Masunga, askari 20 kati ya 414 waliopandishwa vyeo nchini.

SF Labani alisema simu hizo zimekuwa zikisababisha upotevu wa muda na kushindwa kuwahudumia wenye uhitaji wa kweli katika kazi zinazofanywa na jeshi hilo.

"Niwakumbushe tu namba 114 tunatakiwa kupiga wakati wa dharura tu na ukiwa na dharura usianze kuwatafuta ndugu wala kuzunguka kwa watu wengine. Wewe piga simu kwa wakati ili tuone namna ya kufika eneo la tukio na kutoa msaada," alisema SF Labani.

Pia alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakipiga simu na kufanya mzaha wakiomba kuunganishwa 'Freemasons' wengine wakitaka wachumba wakati kuna Watanzania na wenye shida za kweli kama nyumba na maduka kuungua, hivyo kukosa msaada kutokana na simu kutumika kwa mambo yasiyo na maana.

Katika hatua nyingine, Kamanda Labani alisema jiografia na ujenzi holela vimekuwa vikwamisha kuzifikia nyumba zilizopatwa na majanga.

"Nyumba zimebanana hazijajengwa kwa utaratibu, Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007 ikisomwa pamoja na marekebisho yake namba 8/2021, inatoa maelekezo kwamba ramani zote zinatakiwa kuletwa jeshi la zimamoto kabla hazijapewa kibali," alisema.

Pia aliwataka wanaohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi kuacha kutoa vibali kabla ya kuthibitisha kama ramani husika zimesomwa na jeshi hilo ili kulinda usalama wa anayejenga.

Koplo wa Zimamoto Epiana Lutufyo, mmoja wa askari waliovalishwa vyeo, aliahidi kuongeza juhudi katika kuhudumia wananchi, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya matumizi ya namba ya dharura katika kuboresha utoaji huduma.




Rais na Ofisa Mtendaji wa Barrick, Mark Bristow (katikati), akizungumza na waandishi wa habari katika mgodi wa North Mara, wilayani Tarime jana, wakati akielezea mafanikio yaliyopatikana tangu ianze kufanya kazi na serikali kupitia kampuni ya Twiga. Kushoto ni Meneja wa Barrick nchini, Melkiory Ngido na Naibu Waziri wa Madini, Stephen Kiruswa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanri ataja chanzo kuporomoka bei pamba

**Na Alex Sayi,** MASWA

BALOZI wa Pamba nchini, Aggrey Mwanri, ameeleza sababu za kushuka kwa bei ya zao hilo duniani katika msimu wa kilimo 2022/23 kuwa ni janga la UVIKO-19 lililochangia wakulima wengi kuacha.

Pia amesema kutokana na kupungua kwa tishio la janga la UVIKO-19 duniani, nchi nyingi zimerejea kwenye uzalishaji wa zao hilo, hali iliyosababisha soko kuwa na zao hilo kwa wingi na kuathiri mwenendo wa bei ya pamba.

Alitoa ufafanuzi huo juzi wakati akizungumza na wakulima katika Kijiji cha Dodoma Kata ya Mwamashimba, Maswa Mkoani Simiyu, akiwa ziarani kuwaelimisha wakulima namna bora ya uvunaji wa pamba yenye ubora itakayoshindanishwa kwenye soko la dunia.

Pia aliwataka wakulima kuzingatia sheria na kanuni za kulima zao hilo ili kupata tija hata wakati ambao bei ya zao hilo itashuka duniani lakini ubora ukawa si mzuri.

"Ziko sheria kumi za pamba zizingatieni ili uzalishaji wenu uwe na tija ekari moja ikilimwa kitaalamu inatoa kilo 2,500, kwa kufuata vipimo mstari kwa mstari ni cm 60, mche hadi mche sentimita 30 shamba liandaliwe mapema masalia yang'olewe na kuyachoma," alisema Mwanri.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, aliwataka maofisa kilimo, watendaji ngazi za wilaya na vijiji kusimamia sheria za ulimaji wa zao hilo na kutoa elimu kwa wakulima ili kulima kilimo cha manufaa tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Maisha Mtipa, aliwataka wakulima kuzingatia maelekezo waliyopewa na balozi wa zao hilo, ili kunufaika na kilimo hicho. Alisema halmashauri itasimamia maelekezo yaliyotolewa ili kuwa na kilimo chenye tija.

Ofisa Mazao Wilaya ya Maswa, Mabula Yohana, alisema halmashauri hiyo imevuka lengo lililokusudiwa kwenye uzalishaji wa zao hilo la kimkakati kutoka ekari 87,438.06 sawa na asilimia 106.35 kati ya ekari 82212.4 zilizokusudiwa kwa mwaka wa kilimo 2022/23.

## CWT: Mchango wa Mwenge ni hiari

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

MWENYEKITI wa Chama cha Walimu Walimu (CWT), Wilaya ya Karagwe, Joseph Lumulo, ametoa ufafanuzi kuhusu malalamiko ya baadhi ya walimu wilayani humo, kutozwa fedha kwa ajili ya shughuli za Mwenge kwamba michango hiyo ni hiari na sio lazima.

Akiongea jana na Nipashe kuhusu malalamiko hayo alisema michango hiyo ni hiyari na kwamba sio kwa walimu pekee bali hata wananchi wa kawaida.

Lumulo alifafanua kuwa mtumishi wa umma sio kujitenga na jamii endapo ipo shughuli inayohitaji michango kwa ajili ya maendeleo ya serikali anatakiwa kujitoa bila manung'uniko, ili kufanikisha shughuli inayomuhitaji kushiriki pia.

"Uchangiaji wa shughuli za Mwenge ulitolewa kwa wananchi wote, ikiwa ni pamoja na walimu na wala siyo lazima kutoa michango hiyo lakini kwa kutambua umuhimu na ushiriki wako katika jamii unaweza kuamua kutoa au usitoe," alisisitiza.

Aliendelea kusema kuwa yapo mashirika yamepewa jukumu la kutoa kiasi cha Sh.100,000 mengine Sh.50,000 huku walimu wakuu wao wakitakiwa kuchangia Sh.5,000 na kuendelea na walimu wa kawaida Sh. 3,000, huku akiwataja wanaolalamikia michango hiyo kutokuwa na uzalendo.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Burugo, Kata Bugene, Hussen Muhamed, alisema kuwa siyo mara ya kwanza kutakiwa kutoa kiasi hicho cha fedha, kwa kuwa kila shughuli za Mwenge zinapoanza wao pamoja na wananchi wote hutakiwa kufanya hivyo.

Alisema jukumu hilo inapatiwa shule kama shule huku ikipewa pia kiasi cha kuchangia hivyo mwalimu mkuu pamoja na walimu wake wanapanga kiasi cha kutoa, ili kuhakikisha wafika lengo walilowekewa kisha michango hiyo kuiwasilisha wilayani.

Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Julius Laizer, aliiambia Nipashe kuwa michango hiyo ipo kulingana na uwezo wa mtoaji ambaye ni mwananchi yeyote yule bila kujali yeye ni mtumishi au la lengo, likiwa ni kufanikisha shughuli za Mwenge.

Aidha, alisema endapo kuna nguvu inatumika katika kukusanya michango hiyo wasisite kutoa taarifa katika ofisi yake kwa ajili ya kutambua nani anafanya hivyo achukuliwe hatua stahiki.



Ukurasa 12

**POLISARIO na miaka 50 ya harakati za ukombozi**



Ukurasa 13

Kuelekea uchaguzi S/Mitaa, Mkuu 2025 Mwanza inapotangaza ushindi mapema



Ukurasa 14

**EMMANUEL SULTANI MAKENGA Mbabe M23 anayemtunishia Rais DRC misuli, kuwa hawataweka silaha chini**


# siasa

JUMATANO JULAI 12, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MJADALA BANDARI

# Tanzania inaweza kuviunda vielee ni kujiamini, kuthubutu hata DP haijaota

**Na Dk. Felician B. Kilahama**

NI kweli Tanzania inahitaji maendeleo na ufanisi mkubwa katika kuziendesha bandari zake, lakini kubwa la kujiuliza ni je, hayo nchi inayoyahitaji kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kupata faida kwa kutumia kampuni za kigeni, sisi kama taifa hatuyawezi?

Tanzania ina rasilimali ardhi, nguvukazi ya kutosha, siasa safi na uongozi bora inapaswa kujihoji ni nini kinakwamishwa isizimudu bandari zake kwa ufanisi mkubwa?

Tangu ipate uhuru, miaka 62 imepita, bado inahangaika. Lakutafakari ni je, kampuni kama 'DP World' kutoka Dubai, wametumia miaka mingapi kufikia umahiri walionao kiasi cha kutuaminisha kwamba wataisaidia serikali kupata mapato zaidi kuliko hali ilivyo leo?

Ni sawa, sikatai, inawezekana ikawa hivyo ila najiuliza imewachukua muda gani kujijengea umahiri na uwezo walionao leo? Au waliamka siku moja wakajikuta wako hivyo?

Miaka 62 ya uhuru wetu ni mingi tuweza kupiga hatua kimaendeleo ikiwamo uwezo wa kuzimudu bandari zetu kwa ufanisi mkubwa. Nasema hivyo kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni taifa kubwa, tajiri lenye rasilimali na fursa nyingi sana. Mfano, kuwepo bandari kadhaa nchini, ni fursa muhimu kimaendeleo tujiulize tumekwama wapi na tuchukue hatua.

Ndani ya miaka hiyo tumeongozwa na awamu sita je, hali ya maisha kwa walio wengi tukiangalia visababishi ni nini? Tujiulize tunafeli wapi ni siasa, uongozi, kutokuwa na vipaumbele sahihi, matumizi pengine mabaya ya rasilimali fedha na nguvukazi, ukosefu wa wataalamu mahiri, ubinafsi uliokithiri au ni nini hasa?



Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

Tuangalie mataifa kama China, Singapore, Malaysia, THauland, Korea Kaskazini, India, Brazil, yamefanyaje kufikia hali waliyonayo kimaendeleo na imewachukua muda gani wakati takribani miaka 50 iliyopita hawakuwa hivyo?

Ipo nadharia kuwa binadamu wote tunazaliwa sawa ingawa mazingira yanaweza yakatofautiana kidogo kutokana na hali ya kimaumbile. Kiufupi, binadamu anao uwezo mkubwa wa kufanya mambo mengi kujiletea maendeleo kimwili, kiakili, kiafya, kiuchumi, kimiundombinu, kiteknolojia, kijamii, kiutamaduni na kadhalika.

Hata hivyo, uwezo unajengwa tangu awali na unahitaji kuboreshwa au kunolewa kiuendelevu kuwezesha kuyamudu mazingira kwa faida ya wengi. Tunapoisifia 'DP World' kwa ufanisi wake naamini haikuwa hivyo wakati inaanzishwa.

Lakini, kwa umakini waliokuwa nao na kwa misingi mahiri ya 'utashi mkubwa wa kisiasa' katika taifa lao, wakajiendeleza na kufikia hali waliyonayo sasa hadi kuwa "kampuni mahiri duniani" kutokana na ujuzi, maarifa, teknolojia na usimamizi madhubuti.

Inaelezwa kuwa kwenye bandari wanazohudumia hakuna wafanyakazi wengi kutokana na kazi kubwa kufanywa na mashine na kwa haraka sana. Sikatai kwa wao kuwa na ufanisi huo, ila najiuliza walizaliwa nao? Jibu ni hapana.

Ni jambo walilolijijengea umahiri kupitia mbinu mbalimbali, sheria, taratibu, usimamizi na kuwaendeleza watu wao hadi kuwa tishio kiasi hicho.

Kuna usemi "usione vyaelea vimeundwa" havielei tu vimehangaikiwa kwa kiasi kikubwa na kwa kutokwa jasho sana pamoja na kutumia rasilimali kuanzia, fedha, watu na muda kwa umahiri na weledi bila ubabaishaji.

Watanzania tujiulize kwa miaka 62 ya uhuru tumekwama wapi kimaendeleo? Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, baada ya uhuru alisema: Maadui wakubwa wa taifa letu ni "umaskini, ujinga na maradhi".

Kadhalika, akaongeza kuwa ili kuweza kupambana na maadui hao taifa linahitaji ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora, hayo yakawa ndiyo masuala ya kuzingatiwa, je, iwapo ardhi ipo ya kutosha, watu wapo (nguvukazi), siasa safi ipo na uongozi bora je, kwa miongo hiyo tumekwamishwa na kitu gani kiasi cha 'maadui' hao kuendelea kuwepo?

Jitihada, kwa kiasi fulani zimekuwa zikifanyika, lakini siyo za kuridhisha. Kinachotakiwa ni kuongeza nguvu na maarifa zaidi na kuainisha vipaumbele sahihi pamoja na kuujenga uwezo wetu kitaaluma na kiteknolojia.

Wakati wa uongozi wake Mwalimu Nyerere, aliahirisha kuchimba madini akisema 'acha kwanza tujijengee uwezo stahiki tukishakuwa nao tutachimba'.

Aliongeza kuwa wataalamu kutoka nje wakija 'watatulalia' kutokana na masilahi yao kuwa makubwa. Vilevile, aliwahi kusema tusitegemee sana fedha kama msingi wa kujiletea maendeleo bali 'ziwe matokeo ya juhudi na kazi za mikono yetu pamoja na kutumia akili na maarifa ipasavyo'. Ninachofahamu, serikali huendesha shughuli zake kutokana na 'kodi' na 'tozo' kwa watu wake.

Hivyo, itumie sehemu ya mapato hayo kuwaendeleza watu, kadhalika, matokeo mazuri ya serikali madarakani yapimwe ni kwa kiasi gani imejitahidi kuwaendeleza watu wake katika kupigana na 'umaskini, ujinga na maradhi' kwa kutumia vizuri rasilimali na fursa zilizopo nchini.

**INAENDELEA UK. 13**

# POLISARIO na miaka 50 ya harakati za ukombozi




Baadhi ya askari wakiandamana kusherehekea miaka 50 ya POLISARIO. **PICHA: UBALOZI WA SAHARA MAGHARIBI**

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya zaidi ya miaka 60 ya uhuru wa mataifa mengi ya Afrika, upo mshangao kwamba bado kuna nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU), ni mkoloni anayeikalia kimabavu Sahara ya Magharibi.

Ni Morocco mwanzilishi wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), na sasa ni AU, akitawala kwa kuchukua ukoloni kutoka Hispania.

Pengine swali kubwa hapa ni hili, ni zipi jitihada zinazochukuliwa na Afrika na ni nini kinafanyika kuwasaidia ndugu hao wa Sahara Magharibi?

Nipashe ina nakala ya waraka wa baadhi ya watetezi wa watu wa Sahara kutoka Ubalozi wa Saharawi jijini Dar es Salaam, wanaoutoa baada ya maadhimisho ya miaka 50 ya POLISARIO Front Movement, yakifanyika hivi karibuni mjini Auserd Jamhuri ya Saharawi.

Katika waraka huo POLISARIO inakumbusha juhudi za viongozi wapigania uhuru kama Julius Nyerere, Kwame Nkrumah wa Ghana, Ahmed Ben Bella wa Algeria na Nelson Mandela wa Afrika Kusini waliofanyakazi kubwa kuondoa ukoloni.

Watetezi hao wanahoji iwapo wangeinuka kutoka makaburini leo wangeshangaa kiasi gani kuona bado kuna ukoloni?

Wangeumia kwa kukuta mwanachama wa AU amegeuka mkoloni kutawala wenzake na pengine wangeendelea kulaani.

Maofisa wa utetezi wa Saharawi katika wanasema kinachotokea Sahara Magharibi ni ukatili na ukiukwaji wa haki za raia.

"Ni makosa ya ukoloni ndani ya bara moja kwa Sahara Magharibi kutawaliwa na Morocco. Inasikitisha kuona ikiinyonya badala ya kusaidia na kuunga mkono juhudi za maendeleo."

Wanasema kinachoendelea katika ardhi ya Sahara Magharibi ni uhalifu dhidi ya ubinadamu na Afrika, mashirika ya kimataifa na dunia hazinabudi kupaza sauti kuiunga mkono ili koloni hilo la mwisho Afrika liwe huru.

Hivi karibuni POLISARIO Front Movement, iliadhimisha miaka 50 ya harakati za kupigania uhuru wao, mjini Auserd, ambako, Rais wa Sahara Magharibi, Brahim Ghali, anahutubia akieleza harakati zao hadi kufikia miaka 50 sasa.

Anasema, "Algeria na Rais wake Abdelmadjid Tebboune, wamethibitisha msimamo wao kwa kukubaliana na katiba na maazimio ya Umoja wa Mataifa(UN) na sheria ya katiba ya AU na hasa kwa kanuni na maadili ya mapinduzi ya Novemba mosi 1954. Shukrani zangu kwake watu wa Algeria."

Anaisifu Afrika kwa kuzingatia nia ya Saharawi kama sababu ya haki ya Kiafrika. Pia anatoa salamu kwa vyama vyote vya ukombozi wa Afrika kwa mapambano ya ukombozi dhidi ya ukoloni ambayo yamewaunganisha.

### JUHUDI ZA UTETEZI

Ikumbukwe kwamba mwezi Septemba 2022 Mahakama ya Haki ya Umoja wa Ulaya ilitoa hukumu kwa Umoja wa Ulaya (EU) kuacha kutumia mikataba ya biashara na uvuvi na Morocco ambayo inadaiwa inalikandamiza taifa la Sahara Magharibi.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na mahakama hiyo, ilieleza kuwa POLISARIO ina uwezo wa kuwawakilisha watu wa Saharawi mbele ya mahakama za Ulaya.

Haki ya watu wa Saharawi kupata kibali haijaheshimiwa, mahakama ilisema. Pia iliongeza kuwa kwamba EU haingeweza kuchukua nafasi ya "ridhaa" ya watu wa Saharawi kwa hoja ya "manufaa".

"Kwa kuzingatia dhana ya kisheria ya watu na ridhaa, "mashauriano ya watu walioathiriwa" yaliyoandaliwa na taasisi hayakuweza kusababisha kujieleza kwa ridhaa ya watu wa Saharawi", taarifa hiyo ilieleza, kwa ufafanuzi wa hukumu katika kesi namba T-344/19 na T-356/19 kuhusu uvuvi na uamuzi wa kesi T-279/19 kwenye biashara.

"Huu ni ushindi wa haki na kwa watu wa Sahara Magharibi. Tunatumai kuwa nchi wanachama wa EU sasa hatimaye watatii maamuzi ya mahakama, na kuiondoa Sahara Magharibi kutoka kwa mawanda ya mahusiano ya umoja huo na Morocco.

"Ni wakati muafaka kwa EU kuacha kuwa sehemu ya tatizo katika koloni la mwisho barani Afrika, na kuwa sehemu ya suluhu", anasema Sylvia Valentin, Mwenyekiti wa Sahara Magharibi katika kesi hiyo.

Mahakama ilifafanua kwa mara nyingine kwamba Sahara Magharibi haiwezi kuwa sehemu ya makubaliano na Morocco.

### USHIRIKI WA TANZANIA

Watetezi wa Jamhuri ya Saharawi katika Ubalozi huo nchini, wanaiona CCM kuwa ni mmoja wa wapigania uhuru na rafiki mkubwa wa ujumbe wa vuguvugu la POLISARIO, anayeunga mkono harakati za uhuru wa Sahara Magharibi.

Wanasema CCM ina historia ya ukombozi hasa karibu nchi zote za ukanda wa kusini mwa Afrika. Hali kadhalika enzi za kupigania uhuru wa mataifa mengi ya Afrika Tanzania ilikuwa mstari wa mbele katika harakati hizo jambo ambalo linapaswa kurithiwa na kizazi cha sasa na kusaidia harakati za Sahara Magharibi.

> "Huu ni ushindi wa haki na kwa watu wa Sahara Magharibi. Tunatumai kuwa nchi wanachama wa EU sasa hatimaye watatii maamuzi ya mahakama, na kuiondoa Sahara Magharibi kutoka kwa mawanda ya mahusiano ya umoja huo na Morocco.

Wanaeleza uungaji mkono wa Tanzania kwa POLISARIO kuwa ni historia kwa sababu ulikuwapo tangu wakati wa kupigania uhuru wa Tanganyika chini ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ambaye kwa kiwango kikubwa alishirikiana na kiongozi wa Algeria Rais Ahmed Ben Bella.

Novemba mwaka jana Rais Brahimi Ghali wa Sarahawi, alitembelea Tanzania na kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM mjini Dodoma na kuuhutubia akiomba kuimarishwa kwa ushirikiano na udugu wa CCM na POLISARIO.

Pia alisisitiza na kuomba Watanzania hasa kizazi cha sasa kukumbuka wosia wa Baba wa Taifa Nyerere wa kutetea wanyonge na kuunga mkono juhudi za kupigania uhuru wa Sahara Magharibi.

### MIAKA 50 POLISARIO

Mbali na maonyesho ya kijeshi na ya kiraia, maadhimisho ya miaka 50 ya POLISARIO Front Movement, yalihusisha mikutano mingi yenye mada kadhaa na Mei 20 na 21, pamoja na wajumbe wa pande zote zinazohusiana na suala la Saharawi.

Mpango wa sikukuu pia ulijumuisha matukio yanayoangazia fikra za mwanamke wa Kisahrawi pamoja na maonyesho ya kutangaza kazi yaliyotolewa kwa vitabu vilivyoandikwa na waandishi wa Saharawi.

Kwa upande mwingine mkuu wa mkoa wa Auserd , Khira Bulahi, anawakaribisha wajumbe walioshiriki katika kongamano hilo huku akipongeza mchango wao katika kusindikiza mapambano ya wana Saharawi na sababu zake za kudai uhuru, haki na maendeleo, huku akitoa wito wa kuongezwa kwa juhudi za kutetea Saharawi duniani kote.

Aidha, anasisitiza kuhusu mkutano wa Kimataifa wa Mshikamano na Wananchi wa Sahrawi unapania kuanzisha makundi ya mabunge ya mshikamano na wananchi wa Saharawi ikiwa ni hatua itakayoimarisha diplomasia ya bunge katika nyanja zake mbalimbali za kudai uhuru.

Gwaride la kijeshi lililoandaliwa wakati wa maadhimisho hayo ikiwa ni sehemu ya kusherehekea miaka 50 ya kuanzishwa kwa kundi la POLISARIO FRONT na kuzuka kwa mapambano ya kijeshi ya Saharawi lilitamalaki na kuonyesha matarajio ya Wasaharawi likifichua hasa kiwango cha juu cha taaluma na maandalizi mazuri ya vitengo vya jeshi la Jamhuri ya Saharawi pamoja na uwezo wa kisasa zaidi wa vifaa vya kijeshi.

Gwaride hilo lililoanzishwa na vikosi vya askari wa miguu vilionyesha mpangilio na ukamilifu kama askari wanaojituma wakiwa na mitambo, pamoja na vifaa vya huduma za afya, uhandisi na miundombinu, silaha na vifaa vya hali ya juu.

Taaluma hiyo hiyo imeonyeshwa, kwa kiwango cha juu, na vitengo vya vikosi maalumu vya wanawake ambavyo pia vilishiriki kwenye gwaride hilo.

Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa wakati wa gwaride la kijeshi, vitengo vya jeshi la Sahrawi vinapata mafunzo makali zaidi ya kijeshi ili kuwa na ufanisi katika hali zote.

# Kuelekea uchaguzi S/Mitaa, Mkuu 2025 Mwanza inapotangaza ushindi mapema

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

UCHAGUZI wa serikali za mitaa hauko mbali, maandalizi yameshaanza licha ya kwamba kuna madai kutoka kwa wapinzani kuwa hawajafahamu hatima ya ushiriki wao kutokana na kutokuwapo na Tume Huru ya Uchaguzi.

Mwaka 2019 uchaguzi huo uligubikwa na mambo mengi mojawapo ni upinzani kuususia, ulipofanyika Novemba 2019, hatua iliyotokana na madai ya chama kikuu cha upinzani cha CHADEMA kutangaza kuwa asilimia 94 ya wagombea wake walienguliwa.

CHADEMA ilikataa kushiriki kwa sababu kadhaa pia ikilalama kuwa figisu nyingi zimewaondoa wagombea wake kwenye kinyang'anyiro na kwamba vigezo vilivyowatoa walivitilia mashaka.

Mkoani Mwanza vuguvugu la uchaguzi linaanza kuzungumziwa, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa, Omary Mtuwa, anazungumza na Nipashe akisema mengi kuhusu siasa mkoani humo, akitamka kuwa uchaguzi ujao kwa CCM ushindi ni lazima kila kona na kwamba wamejipanga kikamilifu.

Anawaambia wanachama wake kuwa wamejipanga mtaa kwa mtaa, vitongoji, vijiji ili kuwabwaga wapinzani katika ngazi mbalimbali za uongozi na hawana wasiwasi.

Mtuwa anasema, kwanza wao ndiyo chama baba lao kilichoshika hatamu na dola kuanzia ngazi za chini hadi taifa, hawana shaka watashinda kila kona, udiwani, ubunge hadi urais tena kwa kishindo.

Anataja sababu ya ushindi huo kuwa kinachowabeba ni ilani yao ya CCM ambayo imetekelezwa kwa kishindo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na mtangulizi wake John Magufuli.

Anasema wakati wapinzani wao au vyama vingine wakifikiria kufanya kampeni za kitanda kwa kitanda, nyumba kwa nyumba, watu hao hawana nafasi ya kushinda kutokana na janja yao ya kuchafuana majukwaani na kudai huibiwa kura zao pale wanaposhindwa uchaguzi.




Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa, Omary Mtuwazi. **PICHA: MTANDAO**

"Sisi kawaida tunashinda kihalali sababu kila upande wapo mawakala wa kuhesabu kura za kila mgombea kwenye nafasi yake, kama hakuna mawakala upande mmoja mgombea huruhusiwa kuhesabu kura zake mwenyewe, sasa madai ya kuibiwa yanatoka wapi? Anahoji Mtuwa.

Katibu wa CCM anajisifu kuwa CCM husimamia vizuri utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi tofauti na wengine, inapiga vita vitendo vya rushwa anapokamatwa mgombea na kuthibitika ametenda kosa hilo huondolewa katika kinyang'anyiro hicho.

Lakini, hasiti kusema wakati wa Uchaguzi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iko macho kufuatilia ili kuhakikisha inawatia mbaroni watoa na wapokea rushwa, hivyo mambo mengi yameweza kutekelezwa ikiwamo miradi ya maendeleo ya wananchi, akitoa mfano wa elimu, kilimo, maji, mikopo ya kusaidia jamii kuanzia vyuo vikuu, wanawake, wahitaji na vijana.

Anasema mwaka huu kamati za chama hicho zimefanya ziara za kutembelea miradi ya maendeleo ya wananchi katika mkoa na kwenye wilaya za Nyamagana na Ilemela na kuwataka wanachama wake wasihofu wako kwenye eneo salama.

**MSHINDWE WENYEWE**

Mtuwa anawaambia wanasiasa washindwe wenyewe kwa kuwa demokrasia hivi sasa iko huru kwa vyama vyote vya siasa, Rais Dk.Samia alishafungua milango ya uhuru wa kisiasa iliyokuwa imefungwa hata mtoto wa maskini yuko huru kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi mkuu ujao.

Anasema hata yeye kilichomfikisha hapo kwenye nafasi hiyo ya Katibu Mkoa ni juhudi zake binafsi za kupambana na utendaji wake mzuri, sio mtoto wa tajiri bali ni wa kutoka familia maskini aliyeweza kupigana kishujaa hadi kufikia wadhifa alionao hivi sasa kisiasa.

"Niseme kutafuta uongozi ndani ya chama chetu ni sehemu ya mazoezi kujipima uwezo, mnyonge na maskini wote ni sawa, ndiyo maana hadi sasa Mwanza, tuna wanachama wa CCM 1,101,258," anasema Mtuwa.

Akiwazungumzia wanachama waliohamia CCM kutoka vyama vingine vya siasa kuanzia Januari mwaka huu anasema wanafikia 734,448 akidai wamerejea nyumbani na kwamba wale walikuwa wanajifunza siasa.

**KUSHINDWA MAPEMA**

Anawaambia wapinzania kuwa baada ya kufunguliwa minyororo ya uhuru wa kufanya siasa, wapinzani hawatakuwa na jipya la kusema zaidi ya kusubiri kuwachafua jukwaani, hivyo kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani, vitongoji na vijiji wao watafanya kampeni kupitia mikutano ya hadhara na si vinginevyo.

Kuhusu madai ya vyama vya siasa hususani upinzani, kusema havitashiriki chaguzi zijazo za serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025, kama haitakuwapo Tume Huru ya Uchaguzi, Mtuwa anawaambia ni kushindwa mapema.

Wakati taifa likielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, wahusika wafahamu kuwa siasa ndiyo maisha. Kuna wanaoita kuwa ndiyo njia ya kufanya maamuzi katika ngazi mbalimbali za vyama, serikalini, jamii na kuwawakilisha wananchi katika shughuli za kimaendeleo, uchumi, lakini pia sehemu ya maisha hivyo wasikate tamaa.

Wengine wanasema siasa ni mchezo mchafu, hugeuka vita hasa nyakati za uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa viongozi wa ngazi za juu, udiwani, ubunge na urais, hugubikwa na fitina baina ya wagombea wanaotafuta nafasi hizo ikiwamo hata kuumizana, lakini lazima ifanyike.

Hakuna sababu ya kuumizana ndiyo maana wapo wanaoeleza kuwa vita vya wanasiasa havidumu, ukiisha uchaguzi wanarudi kuwa marafiki,wanaokula pamoja, kufurahia, kutembeleana, kusaidiana, lakini wapo ambao fitina zao huenda mbali na hata kusababisha kisasi.

Wapo wanaosema na kuamini moja kwa moja kuwa siasa ni maisha katika makundi mbalimbali ya watu wanaojihusisha kuanzia ngazi za chini hadi taifa, wengine wanaona haiwezi kuwasaidia kimaisha wakiiweka kando na kufanya shughuli zingine wanazoamini zinawasaidia kufikia malengo yao ya kila siku.

Ipo mitazamo mingi katika siasa cha msingi ni kila mmoja kushiriki ili siasa zisonge mbele na kuwe na fikra mbadala kwa maendeleo ya nchi.

## Tanzania inaweza kuviunda vielee ni kujiamini, kuthubutu hata DP haijaota

**INATOKA UK. 11**

Mijadala kuhusu matumizi ya bandari inaonyesha kwamba kupitia wawekezaji serikali itaongeza mapato kwa kiwango kikubwa kuliko ilivyo sasa.

Je, inapata kiasi gani sasa na hao wawekezaji wataongeza kiasi gani na wenyewe watabakia na kiasi gani kila mwaka? Iwapo ni kikubwa kutokana na ufanisi mkubwa katika kuisimamia bandari ikatumika ipasavyo ni jambo jema.

Hata hivyo ni vyema kutafakari, ni vikwazo gani vimekuwa, vikizuia Watanzania kutofikia hali hiyo? Kimsingi tunaweza kufikia kiwango hicho, kinachotakiwa, jibu ni ndiyo kwa kuhakikisha uwepo wa 'utashi mkubwa wa kisiasa' pamoja na juhudi zetu kiakili, maarifa na uweledi katika kutumia na kusimamia matumizi sahihi ya rasilima za taifa.

Naamanisha utashi unaolenga kuujenga uwezo wa taifa kuwa na kampuni na taasisi za kuendesha uchumi hata kutamaniwa na kutafutwa na kampuni au mataifa ya nje ili kutumika kwenye maeneo hayo.

Iwapo serikali itaongeza mapato yake basi ongezeko hilo lianze kutumika kujenga uwezo wa Watanzania kwenye bandari ili mkataba ukimalizika nchi isiyumbe isonge mbele ipasavyo.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema: 'fedha ni matokeo na siyo kigezo kikubwa cha kujiletea maendeleo'. Tukikopa fedha hiyo ni sehemu ya juhudi katika kutumia fursa tulizonazo kupigana na maadui wa taifa kwani kinachokopa kitarejeshwa baada ya juhudi kubwa na jasho katika kujiletea maendeleo.

Tanzania imewekeza katika bandari-Dar-es-Salaam, zaidi ya Shilingi trilioni moja. Kinachotakiwa sasa ni uwepo "utashi wa kisiasa" na dhamira ya kweli kuendeleza bandari zetu. Tujenge uwepo mkubwa wa wataalamu ili waweze kumudu majukumu bila kubabaisha na kazi zifanyike kwa ufanisi mkubwa na haraka.

Ubadhirifu wa fedha na mali za umma na za bandari usijitokeze. Sheria, kanuni, adhabu na taratibu ziwe kali na kutekelezwa ipasavyo.

Viongozi wote kwa misingi ya uongozi na utawala bora, wawajibike kwa wananchi, walipakodi. Akiwekwa mwekezaji ni sawa, lakini awe ni mtoa huduma na wakati huo, akijenga uwezo kwa Watanzania kwa kipindi atakachokuwa amekubaliwa kuwepo na muda ukiisha aliachie taifa utaalamu.

Suala la kujenga uwezo wetu kitaifa lipewe kipaumbe kuliko mengineyo. Maeneo ya kujengea uwezo yaanishwe na yawe sehemu ya makubaliano na kutekelezwa kikamilifu.

Naamini kwa dhamira ya kweli na kwa muda mfupi ujao, Tanzania, kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nje, tutaweza kuujenga uwezo kuyamudu majukumu ya kusimamia na kuwa wahusika wakuu wa maendeleo yetu kutokana na uwekezaji na juhudi zetu wenyewe.

Tutambue vikwazo vilivyopo, tuchukue hatua bila kusitasita wala kutanguliza ubinafsi bali tukizingatia masilahi ya taifa kuliko faida binafsi zinazoongeza ujinga, umaskini na maradhi.

EMMANUEL SULTANI MAKENGA

# Mbabe M23 anayemtunishia Rais DRC misuli, kuwa hawataweka silaha chini



Kiongozi wa M23 Sultani Makenga. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

EMMANUEL Sultani Makenga ( 51), aliyewahi kuwa kanali wa zamani katika Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo- DRC ndiye kiongozi wa waasi wababe wa M23, ambaye karibuni anatunisha misuli kwa wadau mbalimbali wanaotaka amani ya kweli Congo.

Ana shutuma au lawama nyingi, kwanza anahusishwa na kupanga mauaji ya raia, kuteka nyara, kutumia ubakaji kama silaha ya vita na kuajiri watoto kwenye jeshi askari.

Aidha, ni mtu anayetafutwa na yumo katika orodha ya waliowekewa vikwazo vya Umoja wa Mataifa na Marekani.

Ndiye kiongozi wa M23 ambao ni waasi waliounda kundi maarufu liitwalo March 23 Movement (M23), lakini linalojulikana kama Jeshi la Mapinduzi ya Kongo.

Linadaiwa liliundwa na wanachama wa zamani wa waasi wa the National Congress for the Defense of the People (CNDP) ni

> Lakini Makenga, ambaye yuko chini ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwa madai ya uhalifu wa kivita, anatamba kwenye video...

kikosi cha wanamgambo wenye silaha kilichoanzishwa na Laurent Nkunda katika jimbo la Kivu DRC Desemba 2006.

M23 inadaiwa hufadhiliwa na serikali ya majimbo jirani ya Rwanda na Uganda, licha ya viongozi wa nchi hizo kupinga na kukanusha madai hayo.

**UJEURI WA MAKENGA**

Wiki iliyopita, katika video nadra sana kuonekana kwa mujibu wa BBC, kiongozi huyo wa waasi wa M23, Makenga, anapuuzilia mbali kuwa upande wake utaweka silaha chini ili kupata amani.

Anasisitiza kwamba ikiwa serikali inataka amani "kutakuwa na amani" na "kutakuwa na vita" kama wanataka vivyo hivyo.

Anasema hayo mwaka huu umekuwa na juhudi za kupata amani ya DRC na Mei, kama sehemu ya mchakato wa amani mashariki mwa DR viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanasisitiza M23 na makundi mengine ya waasi yanapaswa kupokonywa silaha na kuwekwa katika kambi maalum za kijeshi ili kumaliza mgogoro.

Lakini Makenga, ambaye yuko chini ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwa madai ya uhalifu wa kivita, anatamba kwenye video hiyo kwamba "kuachana na silaha hakutawahusu kwa vyovyote vile".

Hata hivyo, katika ujumbe huo unaousambaza msemaji wa M23, anaeleza kuwa kundi hilo limesikia ombi la wakuu wa nchi la "kusitisha mapigano na kujiondoa" Anaongeza kuwa wanasubiri serikali ikubali kujadiliana nao.

Lakini, Aprili mwaka huu, Rais wa DR Congo Felix Tshisekedi, anaapa hilo "halitawezekana na kuwatolea nje. Baada ya mapigano ya mwaka mzima kati ya Jeshi la Congo na M23, kumekuwa na utulivu katika jimbo la Kivu Kaskazini tangu Machi, baada ya viongozi wa eneo hilo kutoa wito wa kusitishwa kwa mapigano.

Umoja wa Mataifa unasema kuwa zaidi ya watu 500,000 wametoroka makazi yao kutokana na mapigano hayo ya kushtukiza na yasiyokwisha huku lawama zikielekezwa kwa Rwanda zikitoka kwa wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanaolishutumu taifa hilo kwa kutuma wanajeshi wake kupigana pamoja na M23.

Serikali ya Rwanda mara kwa mara imekanusha hili na kusema ripoti hizo zinaeneza upotoshaji hatari na uzushi".

**HISTORIA YAKE**

Kamanda huyo mkuu wa kundi la waasi la M23, Makenga, alirudi mashariki mwa DRC mwaka jana, akitokea nchi jirani ambayo msemaji wa kundi hilo, Willy Ngoma, hakuitaja.

Meja Ngoma akitoa taarifa za kurejea anasema kwamba tangu arudi DRC, Makenga alikuwa akitembelea wapiganaji katika sehemu mbali mbali mashariki mwa nchi hiyo ikiwamo mji wa Bunagana ambao sasa unadhibitiwa na

Vikosi vya Ukanda ya Afrika Mashariki, vilivyotangaza kuwa sasa vinaudhibiti na kwamba ni eneo la kimkakati mashariki mwa DRC ambao hapo awali ulikuwa ukishikiliwa na waasi wa M23 kwa zaidi ya miezi tisa.

Makenga, mwenye umri wa miaka 51, anasemekana kujua vizuri nguvu na uwezo wa jeshi la DRC, na eneo zima la Kivu Kaskazini, kwa mujibu wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika-VOA.

Kanali Makenga anaelezwa kuwa amekulia katika maeneo ya milimani mkoani Kivu Kusini ndani ya Congo, na husifika sana kwa kuwa mlenga shabaha na mtu mwenye maarifa na ujuzi wa kupanga mambo ya kijeshi.

Alipata ujuzi wake wa kijeshi nchini Rwanda, ambako alikuwa mmoja wa wapiganaji wa Rais Paul Kagame, kabla kiongozi huyo hajachukua mamlaka ya urais na kuongoza nchi hiyo.

Baadaye kiongozi huyo wa M23 alirejea DR Congo na kuwa mtu mashuhuri katika harakati za kudai haki za Watutsi wazawa wa Congo ambao pia ni wachache.

Maisha ya Kanali Makenga kama mwanajeshi yanaelezwa kuwa yalibadilika sana wakati wanajeshi wa M23 walipoteka mji wa Goma, Mashariki mwa DR Congo.

Pia anaelezwa kuwa alimshinda hasimu wake wa kijeshi ndani ya M23 Kanali Bosco Ntaganda - na kumtumbua kama kamanda wa wapiganaji hao waasi.

Ntaganda alikimbilia nchini Rwanda ambako alijisalimisha kwa ubalozi wa Marekani, kisha kufikishwa katika mahakama ya kimataifa ya uhalifu, ICC nchini Uholanzi, akafunguliwa mashtaka ya uhalifu wa kivita.

Mnamo Desemba 14, 2022, Ntaganda alihamishwa Ubelgiji kutumikia kifungo chake katika gereza la Leuze-en-Hainaut, baada ya mahakama ya ICC kumpata na hatia.

Licha ya kumwengua Ntaganda, kuna madai kuwa upo msuguano kati ya Makenga na maofisa wengine wa jeshi wa M23 ambao bado wanamuunga mkono Ntaganda dhidi ya Makenga.

Ingawa hakuna kibali cha kumkamata, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilimwekea vikwazo vya usafiri pamoja na kuzuia mali zake, akituhumiwa kwa kuongoza uasi wa M23 na kuwafanyia ukatili raia wa Congo, Mashariki mwa nchi.

Lakini Makenga, ameendelea kujitetea kuwa anapigana vita halali akitetea haki za jamii ya Watutsi.



## Watumishi 463 wapandishwa madaraja manispaa ya Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATUMISHI 463 sawa na asilimia 94 wamepandishwa madaraja katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida hadi kufikia Aprili, mwaka huu.

Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu wa Manispaa hiyo, Kulanga Kanyanga, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa upandishaji madaraja kwa Menejimenti ya Manispaa hiyo.

Alisema watumishi hao waliopandishwa madaraja ni kati ya watumishi 490 waliolengwa.

Kanyanga alisema watumishi hao baada ya kupandishwa madaraja tayari wameshaingizwa katika mfumo wa mshahara.

Alisema usimamizi madhubuti na ushirikiano baina ya watumishi na uongozi umewezesha kufanyika kwa haraka na kwa ufanisi.

Kutokana na ufanisi katika kazi hiyo, alisema kumeiwezesha halmashauri hiyo kupewa tuzo ya ufanisi na usimamizi bora wa masuala ya utawala.

"Siri kubwa ya mafanikio hayo ni ushirikiano uliopo baina ya wakuu wa Idara na vitengo, madiwani na watumishi katika ngazi na sekta zote,"alisema.

Kanyanga alisema mafanikio hayo si tu katika upandishaji madaraja bali pia katika nidhamu kwa watumishi, uzalendo na kujituma katika kazi.

Aliongeza kuwa kutokana na mafanikio hayo kumeanzishwa programu ya kumotisha watumishi wanaofanya vizuri zaidi kila mwezi katika Manispaa ya Singida.

# Waziri aagiza matumizi ya TEHAMA uwasilishaji matamko viongozi umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeagizwa kutumia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kupokea matamko ya rasilimali, maslahi na madeni ya viongozi wa umma ili kuongeza uwazi katika utendaji kazi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alitoa agizo hilo jana alipotembelea ofisi za sekretarieti hiyo jijini hapo.

"Angalieni matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kupokea matamko ya rasilimali, maslahi na madeni ya viongozi wa umma. Hii itasaidia kuongeza urahisi wa viongozi kuwajibika, uwazi na kupunguza minong'ono katika umiliki wa mali kwa viongozi wa umma," alisema.



Alisema matumizi ya TEHAMA yanayokusudiwa yanatakiwa kufungua milango kwa kiongozi wa umma kuongeza rasilimali zao wakati wowote bila kusubiri mwisho wa mwaka.

"Katika matumizi ya mifumo, hakikisheni mnawashirikisha watumiaji kwasababu wao ndio wanaojua changamoto za ujazaji wa tamko," alisisitiza.

Pia alisema muundo wa sekretarieti hiyo unatakiwa kuangaliwa upya ili kuiboresha na kuleta ufanisi katika utendaji kazi.

"Haiwezekani chombo kama hiki chenye historia kubwa kisiboreshwe mara kwa mara ili kuleta ufanisi katika kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Iangalieni upya miundo yenu kama inaleta tija," alisema.

Naye Kamishna wa Maadili, Jaji (Mstaafu) Sivangilwa Mwangesi, alimweleza Waziri kuwa tatizo kubwa la sekretarieti hiyo kwa sasa ni kutokamilika kwa ujenzi wa jengo la makao makuu na ofisi ya Kanda ya Kati ambao umetumia muda mrefu.

"Waziri ujenzi wa jengo letu umetumia muda mrefu sana, kutokamilika kwa jengo letu kunatulazimu kuendelea kufanyia kazi katika jengo la kupanga, kama jengo letu lingekamilika kwa wakati tungeweza kuokoa fedha za pango kutekeleza majukumu mengine," alisema.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba (wa pili kushoto), akizindua rasmi ripoti ya FinScope 2023 jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasisitizwa mbinu kuzuia mafundisho potofu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, amewataka wadau wa kampeni ya serikali ya Linda Maadili kuja na mbinu zitakazozuia watoto kupandikizwa mafundisho potofu.

Mpanju aliyasema hayo juzi katika kikao cha wadau wanaosimamia maadili kwa watoto na jamii kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini kwa kuwakutanisha wataalamu kutoka wizara za kisekta na taasisi mbalimbali.

Alisema mafundisho potofu ambayo hupitia njia mbalimbali ikiwamo mitandao ya kijamii, yana athari kubwa kwa watoto na jamii na kwamba iwapo hayatadhibitiwa athari zake zitasababisha maumivu katika jamii siku za karibuni.

"Haya tunayoyaona leo ya wanadamu wenzetu kujiita Mungu wala hayakuibuka tu bali ni kwa sababu ya mafundisho potofu yaliyopandwa ndani yao. Sisi kama wizara yenye dhamana ya watoto na jamii pamoja na juhudi serikali, tumeona lazima tukutane kwa sababu hili linagusa watoto na kesho ya nchi hii. Tujadiliane, mje na utaalamu wenu tuje na suluhu ya kudumu ya nini hasa tukifanye ili lengo la kuilinda jamii ya kitanzania," alisema.

Mpanju aliongeza kuwa kila mwanajamii, mzazi na mlezi ana jukumu la kuhakikisha anamlinda mtoto na kuzingatia maadili.

Awali, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao, alisema wamekuwa wakitumia kila nafasi kuhimiza suala la kulinda maadili.

"Kila taasisi kwetu tumeona ni fursa kuitumia kufikisha ujumbe na kuigusa jamii lengo letu ni kuangalia watoto wetu wanapata maadili mema kwa kupitia nyanja mbalimbali na fursa mbalimbali zilizopo lakini kwenye njia ambazo zipo hatuanzishi vitu vipya.

"Tunajua makanisa yapo, wanajamii na viongozi wa dini wapo tunachofanya ni kwenda kuhamasisha na kupeleka zile jumbe ambazo sisi tunatamani zisambae," alisema.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Emmanuel Urassa, alisema tayari wameanza utafiti kuangalia nchi zingine zinavyokabiliana na tatizo hilo na kuona ni namna gani wanaweza kuja na sera ya ulinzi wa mtoto mtandaoni ambayo itakidhi mahitaji ya muktadha wa sasa na baadaye.

"Sisi tumeshaanza kuandaa 'Online Child Protection (mfumo wa kumlinda mtoto kwa njia ya mtandao). Pia tumeshafanya utafiti katika mataifa mengine kuona jinsi wao wanafanya kulinda haki za watoto na maudhui yasiofaa ili tutoke na sera moja. Tutahakikisha wale wote ambao wamekuwa wakizalisha maudhui ya mtandao watatakiwa waweze kufuata sera za nchi yetu,"alisema.





# Mbunge awakumbuka wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, amekabidhi viti mwendo kwa baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu katika Wilaya ya Rungwe ili viwasaidie kwenda shuleni na kurudi.

Pia amekabidhi taulo za kike kwa wanafunzi wa kike wanaosoma katika shule mbalimbali za sekondari ili ziwasaidie kujisitiri wanapokuwa kwenye hedhi na kupunguza tatizo la utoro shuleni.

Fyandomo alikabidhi vifaa hivyo juzi wakati wa uzinduzi wa Taasisi yake ya Sima Ikenda Foundation ambayo inahusika na masuala mbalimbali ya kijamii hasa yanayowahusu wanawake, vijana na wazee.

Alisema vifaa hivyo vitawasaidia wanafunzi hao kuhudhuria shuleni na kuhudhuria masomo jambo ambalo litaongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi hao.

"Hapa nakabidhi viti mwendo sita kwa wanafunzi hawa wenye ulemavu ili viwasaidie kwenda shuleni, lakini kuna mabinti zetu ambao hawana uwezo wa kupata taulo za kike nao nawakabidhi taulo ili wakajisitiri vizuri," alisema Fyandomo.

Alisema mbali na kundi hilo la wanafunzi, pia aliandaa mashine za kusaga na kukoboa ambazo atakabidhi kwa ajili ya miradi ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinzuzi (CCM) katika wilaya zote za mkoa wa Mbeya.

Vilevile alisema alitoa kitanda cha kujifungulia na mashuka katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe pamoja na kutoa Sh. milioni moja kwa umoja wa wazee wa wilaya ya Rungwe.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizindua taasisi hiyo, alimpongeza mbunge huyo kwa kubuni taasisi hiyo huku akisisitiza kuwa ina dira ya kusaidia makundi maalumu ambayo yamekuwa yakiachwa nyuma mara nyingi.

Alisema kama yalivyo malengo ya taasisi hiyo, inatakiwa makundi hayo yasaidiwe zaidi kwa ajili ya ustawi wa jamii hasa makundi ya wazee na watu wenye ulemavu.

Dk. Tulia alimshauri Fyandomo kuendelea kutafuta vyanzo vya mapato ili apanuwe zaidi huduma kwa kufika katika kata mbalimbali za mkoa huo na kuyahudumia makundi anayoyalenga.

"Unapowahudumia wananchi kupitia hii taasisi yako lazima utapokea lawama kwa hiyo lazima uwe mvumilivu na uwe tayari kutumia fedha kama ambavyo umeshaanza kuzitumia kwa kutoa vitu mbalimbali," alisema Dk. Tulia.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, ambaye alishiriki kwenye uzinduzi huo, aliwataka Watanzania kuendelea kudumisha amani.

Alisema taifa linapokuwa na amani mambo mbalimbali ya kimaendeleo ni rahisi kufanyika kuliko kwenye taifa ambalo halina amani na utulivu.

Malasusa alimpongeza mbunge Fyandomo kwa kutoa misaada kwa makundi maalumu akieleza kuwa alichokifanya ni sawa na kutoa sadaka.

Aliwataka viongozi wengine wenye uwezo kuendelea kuyasaidia makundi hayo ili na yenyewe yaendelee kujikwamua kiuchumi huku akiyataka makundi hayo kutumia vizuri misaada.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vivo Energy Tanzania, Khady Sene (kulia), akikabidhi funguo ya pikipiki mpya kwa mshindi wa promosheni ya "Jaza Ushinde Tena na Engen", Michael Kida, mkazi wa Kipunguni jijini Dar es Salaam jana, aliyeshinda baada ya kujaza mafuta kwenye vituo vya Engen. Wengine ni Muuzaji wa Kituo cha Kipunguni, Muslim Baruani (wa pili kulia) na Meneja wa Mauzo ya Rejareja, Adams Ouedrago. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC Malisa apigia debe maonyesho Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kuchangamkia fursa ya maonyesho ya kimataifa ya kilimo (Nanenane) ambayo yanatarajiwa kufanyika kwa mara ya kwanza mkoani hapa kwa kuboresha huduma wanazozitoa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliyesema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo alipokuwa anasikiliza kero na kukagua miradi ya maendeleo.

Miradi aliyokuwa anakagua Malisa ni ile ambayo inatarajiwa kupitiwa na Mwenge wa Uhuru ambapo katika ziara hiyo aliambatana na baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama.

Alisema wamiliki wa hoteli wanatakiwa wajiandae kupokea wageni wengi kwenye maeneo yao na hivyo ni muhimu wakaboresha zaidi huduma zao.

Alisema maandalizi yameshaanza ikiwa ni pamoja na vikao vya maandalizi, ukusanyaji wa michango kutoka kwa wadau pamoja na waonyeshaji mbalimbali watakaoshiriki.

Vilevile alisema wanaendelea na maboresho ya miundombinu mbalimbali katika Uwanja wa John Mwakangale ambao ndio unatumika kwa maonyesho hayo.

Alisema miundombinu ambayo inaboreshwa ni barabara, majengo, miundombinu ya maji pamoja na umeme ili kuhakikisha shughuli hiyo inafanyika vizuri na kwa tija zaidi.

"Baadhi ya mataifa yameshaahidi kushiriki ikiwamo India ambayo Balozi wake tulikuwa naye hapa na aliahidi kampuni zao kubwa kuja kuonyesha bidhaa zao hapa, kwa hiyo wananchi wa Mbeya hii ni fursa kwao," alisema Malisa.

Aidha alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo inaendelea na maandalizi mbalimbali ya kuhakikisha hali ya amani inaimarika wakati wote ikiwemo kipindi cha maonyesho hayo.

# Vyuo vyasisitizwa kuajiri wakaguzi hesabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VYUO vya watu binafsi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, vimeshauriwa kuajiri wakaguzi wa hesabu wa ndani na kutumia ushauri wanaotoa ili kuepuka matatizo ya kifedha kwenye uendeshaji wa vyuo hivyo.

Msaidizi wa Mkuu wa Kanda hiyo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Japhet Simpepo, alitoa ushauri huo juzi wakati wa uzinduzi wa bodi mpya ya Taasisi ya Sayansi za Afya Mbalizi.

Taasisi hiyo inayomilikiwa na Kanisa la Uinjilisti Tanzania ndiyo inayoendesha Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya ya Ifisi, chuo cha afya, shule za sekondari na msingi pamoja na taasisi zingine ndogo.

Simpepo alisema taasisi nyingi za vyuo zinazomilikiwa na watu binafsi hazioni umuhimu wa kuwa na wakaguzi wa ndani kwa sababu akaunti za vyuo zinamilikiwa na wenyewe hali ambayo inasababisha wakuu wa vyuo kutofahamu mapato ya taasisi.

Alisema baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikipata hati zenye mashaka kutokana na hesabu zao kutoandaliwa vizuri pamoja na kuwapo kwa makandokando kwenye matumizi ya fedha.

"Uwapo wa bodi hizi ni takwa la kisheria kulingana na mwongozo wa serikali, hivyo tunatoa ushauri kwa wakuu wa taasisi hizi waziamini mamlaka wanazozipa mamlaka kisheria zikiwamo bodi za ushauri," alisema Simpepo.

Alisema wakati mwingine bodi za taasisi hizo zimekuwa zikikosa nguvu kwenye masuala ya kifedha kutokana na akaunti kumilikiwa na wenyewe vyuo ama wakuu wa taasisi.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Unjilisti Tanzania, Mchungaji Jacobo Mwakasole, alisema wanatekeleza agizo hilo la serikali kwa kuwa na wakaguzi wa ndani na kuhakikisha taarifa zote za kifedha zinawekwa wazi.

Alisema uwapo wa bodi hiyo utawasaidia kuwashauri kwenye mambo mbalimbali yakiwamo masuala ya kifedha hasa kwenye ushauri.

Mkuu wa Taasisi ya Sayansi za Afya Mbalizi, Shukrani Ndumula, alisema taasisi hiyo yenye zaidi ya wanafunzi 1,000 imetoa wataalamu wanaoajiriwa katika taasisi za umma na binafsi.

Alisema wamekuwa wakishiriki pia kwenye uboreshaji wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo ujenzi wa maabara na mabweni kwenye shule mbalimbali za serikali katika mkoa wa Mbeya.

"Kwa sasa tumepewa kibali na Wizara ya Afya kuongeza kozi zingine ikiwamo ya utabibu wa meno na tuko kwenye hatua za ujenzi wa majengo," alisema Ndumula.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Mchungaji Markus Lehner, alisema mafanikio ya taasisi hiyo yametokana na ushirikiano kati yao na wadau mbalimbali ikiwamo serikali na kwamba wameanza ujenzi wa shule na vyuo vingine mkoani Songwe ili kupanua huduma.

Akizindua bodi mpya ya taasisi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliitaka kuwapa kipaumbele wakazi wa eneo hilo kwenye kila huduma wanazotoa huku akiitaka bodi hiyo kuwa na maono.

Aliitaka bodi hiyo kutimiza majukumu yake ipasavyo huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo.

# Watumishi watakiwa kujipima utendaji wao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MADIWANI wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na watendaji wa mabaraza ya manispaa wametakiwa kujitathmini katika utendaji kazi hasa katika uwekaji wa mji safi.

Hayo yalisemwa jana mjini Zanzibar na Mstahiki Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohamed Mussa, katika mkutano maalum wa kampeni ya 'Nipe Fagio' kampeni ambayo imelenga kupambana na uondoshaji wa taka.

Alisema mji wa Zanzibar bado unahitaji jitihada kubwa ili kuwa safi kwa sababu kumekuwapo mipango mingi bila utekelezaji hali ambayo inasababisha mji kuwa mchafu.

Meya Mahmoud alisema tabia hairidhishi hasa katika uwekaji wa mji katika hali ya usafi, hivyo kuwataka kubuni mipango mizuri na kuhakikisha kuwa mji unakuwa safi ikiwamo kujipanga kuongeza watu.

Pia alisema mji kwa sasa ni mchafu licha ya kuwapo mikakati mbalimbali ya kuona mji unakuwa safi. Alisema kwa sasa wamepewa vikosi kusimamia mji ili uwe safi jambo ambalo halipendezi.

"Sisi tuna wajibu gani hata tukawapa vikosi kusimamia usafi wa mji wetu. tujiulizeni, na kila mmoja atimize wajibu wake katika eneo lake huku tukishirikiana na manispaa zetu tukayaondosha majalala yote katika maeneo yote basi mji utakuwa safi," alisema.

Meya huyo alisema madiwani ni hodari lakini haipendezi kuwa kazi zao zinafanywa na masheha, hivyo kufanyiwa kazi na vikosi inaonyesha kuwa hawako tayari kutumiza wajibu wao kama watendaji wa mabaraza.

Pia alisema kiongozi wa nchi amekuwa na imani ya watendaji wake hivyo ni vyema kuendelea kufanya kazi ili kuona lengo lao linatimia katika kuwapatia wananchi maendeleo na kuimarisha mji katika hali ya usafi.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Hassan Mohammed Ali, akizungumzia juu ya uwekaji wa mji safi kupitia mtoa mada juu ya kuona Zanzibar inapiga hatua ya kuweka mji safi, aliwataka viongozi hao kuwa na nia safi na nzuri ya kuona wanadhibiti hali ya uchafu katika mitaa yao bila ya kutegemea misaada mengine.

Alisema inawezekana Zanzibar kupiga hatua ya usafi katika mitaa mbalimbali ikiwa nia na udhibiti wa taka utaendelea kuwa endelevu.

# Zanzibar kuzalisha megawati 48 za umeme jua ifikapo 2024

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MEGAWATI 48 za umeme wa jua zinatarajiwa kuzalishwa Zanzibar ifikapo mwaka 2024, imeelezwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Juma Kilangi, aliyasema hayo jana wakati wa utiaji saini mkataba kwa usimamizi wa ujenzi wa umeme wa jua katika mradi wa ZESTA, Maisara, Mjini Unguja.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuweka mazingira mazuri katika kuwahudumia wawekezaji na wananchi kupitia sekta ya umeme.

Pia alisema megawati 48 za umeme wa jua zitakazozalishwa, zitasaidia kuimarisha na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Kilangi aliyataja maeneo yatakayofikiwa na mradi huo ni pamoja na Makunduchi, Ubago na Matemwe na kwamba umeme huo unaotarajiwa kuzalishwa kupitia kampuni ya GOPA International Energy kutoka Ujerumani, ni chachu ya kukuza uchumi kwenye maeneo hayo na serikali kwa ujumla.

Naye Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Mhandisi Mshenga Haidar Mshenga, alisema kupitia mradi huo watafanya kazi ya ziada ili kuzalisha umeme wa jua katika kipindi hicho.

Aidha, alisema shirika litahakikisha wanafanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na serikali katika kuleta maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa GOPA International Energy Consultant (INTEC), Paul Freunscht, alishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano wa mradi huo wenye lengo la kubadilisha mazingira.

Pia alisema watafanya kila njia ili kupata nguvu ya umeme inayohitajika maeneo hayo ili kutengeneza uchumi wa Zanzibar.



Wanachama wa Chama cha Wananchi (CUF), wakishereheka katika kongamano la chama hicho jijini Zanzibar jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Balozi mpya Uturuki atishwa mzigo

**Na Mwandishi wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amemtaka Balozi Mteule wa Tanzania nchini Uturuki, Iddi Seif Bakari, kwenda kuimarisha mawasiliano na kutekeleza ipasavyo sera ya diplomasia ya uchumi.

Pia amemtaka kuishawishi Uturiki kuanzisha kituo rasmi cha kuunganisha shughuli za wafanyabiashara na biashara Tanzania.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake Migombani mjini Zanzibar, alipokutana na kufanya mazungunzo na Balozi Iddi aliyefika ofisini kwake kumuaga akienda kituo chake cha kazi baada ya kuteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kituo hicho iwapo kitaanzishwa kitaongeza wigo kwa kufanya shughuli zake si tu kwa Tanzania lakini kikafaidisha kanda yote ya Afrika Mashariki, hivyo kusaidia juhudi za nchi katika kukuza uchumi na kuimarisha maendeleo.

Makamu wa Rais alisema Uturuki imepiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa sasa, hivyo ni muhimu kutumia fursa iliyopo ya ushirikiano katika nyanja za viwanda na biashara, elimu na maendeleo ya kijamii kupitia uhusiano uliopo ili nchi kunufaika na kupiga hatua.

Pia alimtaka balozi huyo kutumia uzoefu wake alioupata katika nchi zingine ili wafanyabiashara wa Tanzania kufanya shughuli zao kwa kutumia mfumo na mtindo wa kisasa unaozingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia kuongeza kasi ya maendeleo ya taifa.

Othman alimtaka balozi huyo kuangalia, kuchambua na kuainisha vipaji na taaluma walivyo navyo Watanzania wanaoishi Uturuki ili kusaidia nchi katika nyanja mbalimbali kama zinavyofanya baadhi ya nchi duniani.

Alisema ni dhahiri kwamba wako Watanzania wanaoishi katika nchi hiyo ambao wana vipaji vingi kama vile elimu, ujuzi na maarifa makubwa wanayoweza pia kuyatumia kuyaleta nyumbani kusaidia nchi iwapo wanaunganishwa na kuratibiwa vyema kupitia balozi za nchi wanazoishi.

Naye Balozi Mteule Idd alisema atafanya kila juhudi kuitangaza Tanzania hasa katika sekta ya utalii ikiwa ni pamoja na kufanya ushawishi wa kutumia Shirika la Ndege la Uturuki kuitangaza Tanzania hasa Zanzibar kiutalii kupitia safari za ndege za kila siku.

Aidha, Balozi Idd alisema katika kuendesha biashara ya utalii, kuna haja ya Tanzania hasa Zanzibar kuiga mifumo ya uendeshaji biashara kutoka nchi zingine kwa kupanga na kutenga maeneo maalumu ya biashara hiyo kuepuka mtindo wa kufanya kila eneo nchini kuwa ni la utalii.

Alisema suala la kuitangaza nchi kiutalii hasa Zanzibar litakuwa kipaumbele chake hasa kwa kuzingatia kwamba nchi anayokwenda kuiwakilisha Tanzania inafanya vizuri na kudiriki kukusanya hadi dola bilioni 16 kwa mwaka zinazotokana na utalii jambo ambalo ni muhimu kutumia uzoefu huo kusaidia Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JIMMY WILFRED MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba: **T 575 DDB,** CHASSIS NAMBA: **NCP610081580** na ENGINE NAMBA: **1NZB219747.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/233393/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOKHA SALUM SUWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba: **T 321 BWK**, CHASSIS NAMBA: **AE1105349389** na ENGINE NAMBA: **5AH767620.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/233048/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA. 71 YA 2022**
**STANBIC BANK TANZANIA LIMITED...MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**OLIVA JAMES SADATALLY.....MJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**OLIVA JAMES SADATALLY**

**POPOTE ULIPO**
Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya gharama tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 20/7/2023 saa saba kamili mchana (7:00).

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 6/7/2023

C. M. MAGESA
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GUDILA MODEST TEMU** anatngaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya TVS yenye usajili namba MC 753 DVL, CHASSIS NAMBA: MD625AF48P1B10160 na ENFINE NAMBA: DF4P110132. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/CEN/RB/232758/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANTONIA ANTONI RAPHAEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 309 DZS**, aina ya Toyota **HARRIER**. Chassis no. **ACU300060482**, Engine no. **2AZ0060482**, Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu
Taarifa ya polisi;
**DOD/DOD/RB/232930/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO 69 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MICHAEL TAMBA MANGII of 11**
**Road within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THEAPPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY ROZINA MICHAEL MANGII AND PETER MICHAEL MANGII**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 11 Day of 07, 2023.

**Dated at Dodoma this 25 day of MAY 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARYGLORY PETER ASSEY**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne (form four) chenye namba ya mtihani: **S0269/0054** kilicho tolewa na shule ya Anwarite Girls Secondary School Mwaka 2018, Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha Police kilichokaribu nayeye.
**MOR/MOR/RB/163089/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......11/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MOHAMED RAMADHANI MASUMILO wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HALIMA HAMISI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 18 Mwezi 07 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 05 mwaka 2023

..................HAKIMU..................
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**MAHAKAMA YA TANZANIA.**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya.......KOROGWE**

**Kituo cha ............MANUNDU,.............Mkoa wa TANGA.**

**Shauri la madai Na. ...........11......... /2023.**

**Jina la mdai: ...............................KELVIN DEUS BURITI**

**Jina la mdaiwa: ....................HOSSEIN SAID MKUFYA.**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji Mashauri Mahakama za Mwanzo)**

Kwa **HOSSEIN SAID MKUFYA,** kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii Julai 11,2023 kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama Juni 5, 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MANUNDU - KOROGWE

## KIWANJA KINAUZWA

KIWANJA KIPO **KISUKURU SEGEREA JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA 24 MLABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA NA KINA HATI, BEI NI MILIONI 55. KWA MAWASILIANO **PIGA 0754 857523/0655 857523.**


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Makaburi mengine mapya 40 yagundulika msitu wa Shakahola

**NAIROBI,** KENYA


MAKABURI 40 mapya ya halaiki yamegunduliwa katika msitu mkubwa wa Shakahola nchini Kenya huku awamu ya nne ya shughuli ya uchimbaji ikiendelea.

Waziri wa Usalama wa Ndani, Kithure Kindiki, alisema makaburi 40 ambayo bado hayajafukuliwa yanashukiwa kuwa na miili mingi.

Kindiki vilevile aliendelea kusisitiza dhamira ya serikali ya kukabiliana na wahubiri wahuni.

Akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa Ofisi ya Naibu Kamishna wa Kaunti katika kaunti ndogo ya Igoji, Meru, Kindiki alisema mpango huo unalenga kuhakikisha, hakuna Mkenya mwingine atakayekumbwa na mkasa mwingine kama wa Shakahola.

Idadi ya vifo kutokana na mkasa huo kufikia sasa imefikia 339. **BBC**



Rais wa Kenya, William Ruto, akizungumza kuhusu Sheria ya Fedha inayolenga kukusanya mapato zaidi ili kulipa madeni ya taifa hilo. **PICHA: REUTERS**

## China yashindwa kumtuma waziri wake wa nje Indonesia

**BEIJING,** CHINA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Qin Gang, hatohudhuria mkutano wa kidiplomasia utakaofanyika Indonesia wiki hii kutokana na sababu za kiafya, imeelezwa.

Msemaji katika wizara hiyo, Wang Wenbin ameeleza kuwa badala yake, Mwanadiplomasia Mkuu, Wang Yi, ataiwakilisha China kwenye mkutano huo wa Jakarta.

Mawaziri wa mambo ya nje wa jumuiya ya kusini mashariki mwa Asia (ASEAN) na China wanatarajiwa kukutana mnamo siku ya Alhamisi, siku moja kabla ya mkutano wa kilele wa jumuiya ya Asia ya Mashariki EAS na ASEAN.

Qin, mwenye umri wa miaka 57, alichukua nafasi ya Wang kama Waziri wa Mambo ya Nje wa China mwezi Desemba na alionekana mara ya mwisho mbele ya umma Juni 25, mjini Beijing, baada ya mkutano na maofisa kutoka Sri Lanka, Urusi na Vietnam. **DW**



# Zelensky akerwa muda wa kujiunga uanachama Nato

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ameikashifu Nato, akisema ni "upuuzi" kwamba muda haujawekwa kwa Ukraine kualikwa kujiunga na muungano huo wa kijeshi.

"Ni jambo lisilo la kawaida na la upuuzi wakati muda haujawekwa kwa ajili ya mwaliko au uanachama wa Ukraine," ameandika katika taarifa yenye maneno makali kwenye Twitter.

"Inaonekana hakuna utayari wa kuialika Ukraine kwa Nato au kuifanya kuwa mwanachama wa muungano," ameandika Zelensky.

Nato ilikubali mwaka 2008 kwamba Ukraine "itakuwa" mwanachama. Lakini muungano haukusema namna na lini inaweza kutokea.

"Sasa, tukiwa njiani kuelekea Vilnius, tulipokea ishara kwamba maneno fulani yanajadiliwa bila Ukraine," anaongeza.

Anasisitiza kwamba maneno haya yanahusu, "Mwaliko wa kuwa mwanachama wa Nato, siyo kuhusu uanachama wa Ukraine."

"Kutokuwa na uhakika ni udhaifu. Na nitajadili hili kwa uwazi katika mkutano huo," ameandika kiongozi huyo.

Zelensky alisema bila ya muda wa Ukraine kualikwa kujiunga na Nato, "fursa inaachwa ili kujadiliana kuhusu uanachama wa Ukraine katika Nato katika mazungumzo na Urusi. Na kwa Urusi, hii inamaanisha motisha ya kuendelea na ugaidi wake."

Kyiv imekubali kwamba Ukraine haitaweza kujiunga na Nato wakati vita na Urusi vikiendelea, lakini inasisitiza kuwapo kwa ratiba ya wazi ya matukio.

Baada ya kauli ya Zelensky, Kyiv inakubali haiwezi kujiunga wakati huu wa vita, kwa sababu lazima nchi za Nato zilinde kila mwanachama.

Lakini washirika wa Nato wanazozana kuhusu uanachama wa Ukraine wakati uvamizi wa Urusi utakapomalizika.

Uingereza inataka ifuatiliwe haraka na mataifa ya Baltic na mataifa ya Ulaya Mashariki yanataka muungano huo kuweka wazi ni masharti gani zaidi Ukraine inahitaji kuafikia.

Lakini washirika wengine, pamoja na Marekani na Ujerumani, wako makini zaidi wakitaka Kyiv ikabiliane na ufisadi, iimarishe mahakama na kuhakikisha udhibiti wa kiraia juu ya jeshi kwanza.

Wao pia wana wasiwasi inaweza kusababisha Nato kuingizwa katika vita.

Katika tukio lingine, Nahodha wa zamani wa manowari ya Urusi ambaye alifanya kazi kama Ofisa wa Usajili Vijana ameuawa kwa kupigwa risasi alipokuwa akifanya mazoezi ya kukimbia polepole katika mji wa Krasnodar Kusini mwa Urusi, kulingana na vyombo vya habari vya ndani.

Stanislav Rzhitsky (42), alipigwa risasi na kufariki siku ya Jumatatu na mtu asiyejulikana, shirika la serikali la Urusi



Rossiya 1 liliripoti.

Vyombo kadhaa vya habari vya Urusi vilisema kuwa huenda alifuatiliwa kupitia wasifu wake kwenye programu ya mazoezi ya mwili ya Strava.

Mamlaka ya Urusi imeanza uchunguzi kuhusu mauaji hayo.

Kamati ya Uchunguzi ya nchi hiyo, sawa na FBI ya Marekani, ilisema uchunguzi wa mauaji umeanzishwa na kwamba maofisa watajaribu "Kuweka mazingira yote ya tukio hilo, pamoja na mtu aliyefanya uhalifu na nia yake."

Ofisa huyo wa zamani wa Jeshi la Wanamaji alipigwa risasi mgongoni na kifuani na mtu mwenye bunduki ambaye hakujulikana jina lake alipokuwa akikimbia asubuhi kwenye bustani karibu na kituo cha michezo cha Olimp, gazeti la kila siku la Urusi la Kommersant liliripoti. **BBC**

HABARI MICHEZO

# TPBRC YATAKA LESENI KWA MABONDIA, MAPROMOTA

**Na Abdallah Mataka**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), imetoa miezi miwili kwa mabondia, mapromota na washereheshaji wa mchezo huo nchini kuwa na leseni zitakazowatambulisha.

Makamu wa rais wa TPBRC, Nassoro Chuma, alisema wahusika wa mchezo huo wanapaswa kuwa na leseni za utambuzi, lengo likiwa kuzuia watu wasiokuwa rasmi kujipenyeza na kuharibu wasifu wa masumbwi.

Chuma alisema leseni hizo zenye lengo pia la kutambua idadi ya mabondia, mapromota na washereheshaji wa mchezo huo, zimeanza kutolewa tangu mwanzoni mwa mwezi huu kikomo kikiwa ni Septemba Mosi, mwaka huu.

"TPBRC haitamtambua bondia ama promota yeyote asiyekuwa na leseni na haitamruhusu kufanya kazi hadi atakapokidhi vigezo vya kuwa na leseni.

"Tunataka kuendelea kuufanya mchezo wa masumbwi kuwa wa heshima, shirikisho halipo tayari kufanya kazi na watu wasiokuwa na sifa ambao wengi wao ni waharibifu," alisema Chuma.

Aliongeza kuwa leseni kwa mabondia itatolewa kwa ada ya Sh.10,000 huku mapromota watakiwa kulipa Sh.50,000 na washereheshaji Sh. 20,000.

Katika hatua nyingine, Bondia Ibrahim Class, amewataka mabondia kuitumia nafasi hiyo ya kuwa na leseni ili waweze kutambulika na shirikisho la mchezo huo.

"Ukiwa na leseni ikitokea hata umepata changamoto yoyote ni rahisi kupata msaada kwa sababu unakuwa tayali unafahamika na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa, vile vile itasaidia mabondia kuwatambua mapromota sahihi wakufanya nao kazi," alisema Class.



Kocha wa viungo wa Azam FC, Mfaransa Jean-Laurent Geronimi, akiwanoa wachezaji wake katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendea nchini Tunisia kujiandaa na msimu mpya. **MPIGAPICHA WETU**

# Precision yaidhamini tena Singida FG

**Na Saada Akida**

KLABU ya Singida Fountain Gate FC imeboresha mkataba wao kwa mwaka mmoja zaidi na Kampuni ya Shirika la Ndege la Precision, ukiwa na thamani ya Sh. milioni 118 kwa msimu wa 2023/24.

Awali, kampuni hiyo iliidhamini timu hiyo kwa mkataba wa mwaka mmoja wenye thamani ya Sh. milioni 100 ambao umefikia tamati hivyo kuingia makubaliano mapya.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Precision, Patrick Mwanri, alisema makubaliano yao yapo katika usafirishaji wa timu hiyo katika safari zao zote ndani na nje ya nchini.

Alisema katika makubaliano yao hayo wametoa punguzo la asilimia 50 kwa safari na kutoa tiketi za Sh. milioni 48 katika safari mbaimbali ya ndani kwenye mashindano yao.

"Lakini kutakuwa na punguzo la asilimia 20 sawa na Sh. milioni 70 kwa wale wanaojinunulia tiketi kwa wafanyakazi wa timu hiyo, jumla utakuwa na thamani ya Sh. milioni 118 za Kitanzania na msimu uliopita ulikuwa Sh. milioni 100," alisema Mwanri.

Kwa upande wa rais wa Singida Fountain Gate FC, Japhet Makau, alisema wanathamini ushirikiano na shirika hilo na watahakikisha hawatawaangusha na kuendelea kufanya vizuri katika mashindano yaliyopo mbele yao.

"Tunashukuru kwa sapoti yao kwa msimu uliopita na sasa hatutawaangusha wadhamini wetu kwa kuendelea kufanya vizuri kwa sababu tumefanya usajili mzuri kwa ajili ya msimu ujao," alisema Makau.

## Bares atua Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa FC, imemtangaza Mohamed Abdallah 'Bares', kuwa kocha mkuu wa timu hiyo akichukua nafasi ya Abdul Mingange, aliyeipandisha daraja.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo iliyopanda Ligi Kuu hivi karibuni, inasema kuwa kocha huyo atakinoa kikosi hicho kikiwa kinacheza ligi hiyo kwa mara ya kwanza.

Awali, Bares alikuwa kocha wa Prisons ambapo aliiwezesha timu hiyo iliyokuwa inashika mkia kwenye Ligi Kuu kumaliza ikiwa ya nane msimu uliomalizika.

Akizungumza baada ya kutambulishwa, Bares aliyepewa mkataba wa mwaka mmoja, alisema kazi iliyobaki ni kufanya usajili bora ili timu hiyo iweze kufikia malengo yake.

"Nashukuru Mungu, niko tayari kufanya kazi kwenye Klabu ya Mashujaa, najisikia vizuri kwa sababu mimi ni mwalimu wa mpira, timu yoyote naweza kufundisha, nimekuja huku kwa ajili ya kazi kuifikisha sehemu ambayo tunayoihitaji," alisema kocha huyo ambaye alichukuliwa na Prisons akitokea Mlandege ikiwa ni baada ya kuipa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi mwaka huu.

Alisema yeye kama kocha mkuu, atajipanga na benchi lake la ufundi kutengeneza kikosi cha ushindani, huku akiwataka mashabiki wa Mashujaa FC kuendeleza moto ule ule walioupnyesha wakati timu hiyo ikisaka nafasi ya kupanda Ligi Kuu.

"Kwanza niwapongeze kwa kupanda Ligi Kuu, kingine ni kwamba waendelee kuisapoti timu yao kama walivyofanya wakati wa mapambano ya kuipandisha daraja, kwa upande wetu sisi tumejipanga vizuri kama benchi la ufundi kuona timu yao inafanya vizuri.

"Wakumbuke nao ni wachezaji wa 12, ushirikiano wetu, viongozi na mashabiki ndiyo utatufikisha kule ambako tunataka tufike na kwa upande wa kikosi tutafanya usajili mzuri na wa kuvutia, ila ikumbukwe wachezaji ni wale wale tu, ni kiasi cha kutoa kule na kumleta hapa, kinachohitajika atengenezwe na yeye mwenyewe ajitume awe msaada kwenye timu," alisema kocha huyo.

Mashujaa ilikuwa timu ya tatu kupanda daraja msimu huu kutoka Ligi ya Championship, ikiiondoa Mbeya City kwenye mechi ya 'play off' kwa kuitwanga Mbeya City jumla ya mabao 4-1 kwa mechi zote mbili nyumbani na ugenini.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BEI YA MAGUIRE YATAJWA

Manchester United imeweka thamani inayotakiwa ya pauni milioni 50 kwa klabu inayotaka kumnunua beki wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30. **(Manchester Evening News)**

### WARD-PROWSE AWANIWA

KLABU ya West Ham inatumai kumnunua kiungo wa kati wa England, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 28, kwa ada ya pauni milioni 20, lakini Southampton inataka karibu pauni milioni 40. **(Mail)**

### DOHERTT AKARIBIA WOLVES

WOLVES inakaribia kumsajili tena beki wa pembeni wa Jamhuri ya Ireland, Matt Doherty mwenye umri wa miaka 31, baada ya kuondoka Atletico Madrid. **(TeamTalk)**

### ONANA HUYOOO UNITED

UHAMISHO wa golikipa wa Cameroon, Andre Onana wa pauni milioni 43 kutoka Inter Milan kwenda Manchester United uko katika hatua za mwisho na utakamilika wiki hii baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kukubaliana maslahi binafsi. **(Mail)**

### DE BEEK ANYATIWA

DONNY van de Beek mwenye umri wa miaka 26, pia anaweza kuwa njiani kuondoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto huku Nottingham Forest, Wolves na Crystal Palace zikimtaka kiungo huyo wa kati wa Uholanzi. **(90Min)**

### SPURS UHAKIKA KWA DE VEN

KLABU ya Tottenham Hotspur ina uhakika wa kumsajili beki wa Wolfsburg, Mholanzi Micky van de Ven mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake ni pauni milioni 25. **(Mirror)**

### HEATON KUTUA EVERTON

EVERTON imefanya uchunguzi kuhusu kumsajili mlinda mlango wa zamani wa Manchester United, Tom Heaton, 37. **(Mirror)**

### WAHI ASAKWA SOKONI

MSHAMBULIAJI wa Montpellier, Elye Wahi mwenye umri wa miaka 20, na mshambuliaji wa Juventus raia wa Serbia, Dusan Vlahovic (23), ni miongoni mwa wachezaji ambao Chelsea imeingia sokoni kusaka huduma zao. **(Evening Standard)**

### SCHUURS AFUKUZIWA LIVER

BEKI wa kati wa Torino Mholanzi Perr Schuurs mwenye umri wa miaka 23, anafukuziwa na Liverpool huku kocha Jurgen Klopp akijaribu kuimarisha safu yake ya ulinzi bila kutumia ada kubwa. **(Football Insider)**

### MAXIMIN NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaweza kumuuza winga Mfaransa mwenye umri wa miaka 26, Allan Saint-Maximin - ambaye anasakwa na baadhi ya Klabu za Saudi Aarabia - ili kusaidia kupata fedha za kumnunua nyota wa Leicester City, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 25. **(Telegraph)**

### LEICESTER KWA MAVIDIDI

KLABU ya Leicester City ina nia ya kumsajili mshambuliaji, Stephy Mavididi mwenye umri wa miaka 25, kutoka Montpellier. **(Fabrizio Romano)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KOCHA AMTAKA KANE ASIONDOKE TOTTENHAM

●●●Ni mtu muhimu katika historia ya klabu hii ya soka, nitafanya naye mazungumzo na tutatoka na aina fulani ya uelewa...

**LONDON, Egland**

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, amesema anataka Harry Kane abaki katika klabu hiyo, lakini amekiri kuwa hajapata "uhakikisho wowote" kuhusu hatima ya mchezaji huyo huku kukiwa na ripoti za kutakiwa na Bayern Munich.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Kane, ambaye anaingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Tottenham, ameambiwa kwamba hauzwi msimu huu wa majira ya joto na hakuna mpango wa klabu kumtoa mfungaji wao huyo bora.

Postecoglou, akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wake wa kwanza tangu kuteuliwa kuwa kocha wa klabu hiyo ya Kaskazini mwa London, alisema: "Sidhani kama ni jukumu langu kukaa pale na kuwatendea watu kwa namna kwa sababu ya hali zao. Nitamtendea kila mtu sawa.

"Harry tayari ni mtu muhimu katika historia ya klabu hii ya soka. Yeye ni mmoja wa wachezaji bora. Ninamtaka hapa na ninataka kuifanya klabu hii kufanikiwa. Nina hakika anataka hivyo pia."

Kane anatarajiwa kurejea klabuni kwa ajili ya mazoezi ya kujiandaa na msimu ujao leo, Jumatano na Postecoglou alisema ana nia ya kuzungumza na fowadi huyo.

"Nitafanya mazungumzo ambapo tutatoka na aina fulani ya uelewa," alisema Postecoglou.

"Nataka tu kujitambulisha na ninataka kujua nini anataka kitokee ili kufanikisha klabu hii kisha tutatoka nje ya uwanja wa mazoezi na kufanya hivyo.

"Sijapata hakikisho lolote la yeye kubaki. Kwa hali kama hizi huwezi kushughulika na uhakika. Ninaweza tu kwenda na kile ninachojua hivi sasa. Harry ni sehemu ya kikosi na anasubiriwa kwa hamu."

Postecoglou alitajwa kama kocha mkuu wa Spurs Juni mwaka huu baada ya kuondoka Celtic, ambapo alishinda Ligi Kuu ya Scotland msimu wa 2022-23.

# CHELSEA YAKOMAA NA INTER KUHUSU LUKAKU



**MILAN, Italia**

CHELSEA imeionya Inter Milan kwamba, lazima wakaribia bei wanayohitaji ya pauni milioni 40 kwa mshambuliaji Romelu Lukaku, kwa mujibu wa 90min.

Klabu hizo mbili zimekuwa kwenye mazungumzo juu ya Lukaku kwa miezi kadhaa, huku Chelsea wakikataa ofa kadhaa kutoka kwa Inter na pia wakitafuta kurejesha fedha nyingi iwezekanavyo kutoka kwa uwekezaji wao wa awali wa pauni milioni 97.5 walipomnunua.

Jaribio la Inter kutaka kumsajili tena Lukaku kwa mkopo lilizuiwa haraka na Chelsea, ambao wanataka sasa auzwe jumla.

Ofa ya takriban pauni milioni 30 imekataliwa hivi majuzi na Chelsea, huku vyanzo vikithibitisha kwamba 'The Blues' hao wanashinikiza Inter kuongeza dau lao kwa pauni milioni 10 nyingine.

Inter hawana bajeti kubwa ya uhamisho na kwa hiyo wanania ya kuepuka kutumia fedha nyingi kwa Lukaku, ingawa kuuzwa kwa kipa Andre Onana kwenda Manchester United kunaweza kuwapa 'Nerazzurri' hao nafasi ya kuongeza dau.

Ili kujaribu na kusaidia hatua hiyo, Lukaku yuko tayari kukatwa mshahara mkubwa. Analenga tu kurejea Inter msimu huu wa majira ya joto licha ya kuvutia nia kutoka mahali pengine.

Juventus wameulizia kuhusu Lukaku baada ya Chelsea kuonesha nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa 'Bianconeri' hao, Dusan Vlahovic - moja ya majina mengi kwenye orodha fupi ya wachezaji wanaolengwa na Blues - lakini Lukaku hataki kujiunga na timu nyingine ya Serie A.

Lukaku pia amepoteza nafasi ya kuhamia Saudi Arabia, ambayo ilifanya juhudi mpya kumshawishi mshambuliaji huyo kuelekea Mashariki ya Kati baada ya kuwasili mapema msimu huu wa majira ya joto.

Ofa yao imesalia mezani, lakini Lukaku hataki kukubali huku akisubiri Inter wafikie makubaliano.

# Van de Beek anukia kuondoka Man United

**MANCHESTER, England**

WAWAKILISHI wa Donny van de Beek wamekuwa katika majadiliano na klabu kadhaa za Ulaya kuhusu uwezekano wa Mholanzi huyo kuondoka Manchester United majira haya ya joto, kwa mujibu wa Daily Mail.

Van de Beek alijiunga na United Septemba 2020 akitokea Ajax, lakini hajawahi kupata nafasi katika kikosi cha kwanza cha klabu hiyo chini ya makocha kadhaa.

Van de Beek amekuwa nyuma ya Bruno Fernandes katika safu ya kiungo na amekuwa akipambana na majeraha kadhaa ambayo yamedhoofisha kiwango chake nchini England.

Chini ya Erik ten Hag, kocha wa sasa wa United na kocha wa zamani wa Van de Beek kule Ajax, bado mambo hayajabadilika.

Van de Beek alipata jeraha Januari ambalo lilimweka nje kwa kipindi cha pili cha msimu uliopita na wakati amejiunga na mazoezi ya kujiandaa na msimu katika siku za hivi karibuni, United pia imemsajili Mason Mount kutoka Chelsea - na hivyo kupunguza uwezekano wa Van de Beek kupata nafasi msimu ujao.



Ingawa Ten Hag ana uhusiano mzuri na mchezaji huyo, lakini amewasha taa ya kijani kuondoka kwa Van de Beek kutoka katika klabu hiyo, na kambi ya mchezaji huyo inachunguza wapi atakwenda.

Van de Beek ana klabu kadhaa kutoka Serie A zinazowania huduma yake, huku Inter, Roma na Milan zikiwa tayari kutuma ofa, ingawa inafahamika kuwa yeye si chaguo la kwanza kwa timu yoyote kati ya hizi tatu.

Katika Ligi Kuu England, Wolves, Nottingham Forest na Crystal Palace zote zinafuatilia hali ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

Mabingwa wa Ligi ya Europa, Sevilla na Nice iliyonunuliwa na Sir Jim Ratcliffe, pia zinamwania, sawa na Celtic ya Brendan Rodgers.

# Wasaudia wazidi kumshawishi Pogba

**RIYAHD, Saudi Arabia**

LIGI Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, inaendelea kumshawishi Paul Pogba kutua huko msimu huu wa majira ya joto, ingawa kiungo huyo wa Juventus hajashawishika na kuhama kwa wakati huu, kwa mujibu wa 90min.

Utajiri wa klabu za Mashariki ya Kati umewashawishi wachezaji kadhaa wa hadhi ya juu kufanya mabadiliko msimu huu wa majira ya joto, wakiwamo Karim Benzema, N'Golo Kante, Roberto Firmino na Ruben Neves.


Majina ya nyota zaidi yanatarajiwa kufuatia katika wiki na miezi ijayo, huku Saudi Arabia ikitafuta kuboresha ubora wa ligi yao kabla ya ombi la kuandaa Kombe la Dunia la FIFA la mwaka 2030.

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi (PIF), ambao ndio wamiliki wa Newcastle United, tayari wamemwaga kiasi kikubwa cha fedha katika klabu nne kubwa nchini humo - Al Ittihad, Al Nassr, Al Hilal na Al Ahli - na nia yao ni kuendelea kuvutia wachezaji bora duniani.

90min ilifichua mapema Juni kwamba, Pogba alikuwa mmoja wa watu wenye majina makubwa kwenye rada za PIF na hilo linabakia kuwa hivyo, licha ya kuwa alichezea Juventus kwa dakika 151 tu msimu uliopita kwa sababu ya majeraha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alitembelea Saudi Arabia mwishoni mwa juma, na vyanzo vilithibitisha kwa 90min kwamba mazungumzo yalifanyika na PIF juu ya uwekezano wa kuhamia huko - ingawa alitembelea kwa sababu ya masilahi ya biashara yake binafsi.

Pogba, kwa hali ilivyo, angependelea kubaki Juventus ili kujidhihirisha kwa kocha Massimiliano Allegri - Muitaliano huyo ambaye alimrejesha Turin kwa kipindi cha pili katika maisha yake ya soka.



HABARI MICHEZO

# BARRICK SASA KUJENGA UWANJA WA SOKA MARA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji dhahabu ya Barrick, imeanza mchakato wa kujenga uwanja wa kisasa wa soka mkoani Mara pamoja na kuanzisha timu itakayoshiriki mashindano mbalimbali ya mchezo huo yaliyopo chini ya Shirikisho la Soka Tanzania, TFF.

Akizungumza kwenye mkutano uliohusisha viongozi wa Serikali ya Mkoa, Wizara ya Madini na kampuni hiyo, rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow, alisema tayari wameunda kamati maalum ya michezo ambayo imeanza taratibu za ujenzi wa uwanja huo.

Alisema kamati hiyo imetembelea viwanja mbalimbali ukiwamo Uwanja wa Gwambina uliopo Misenyi ili kuangalia namna bora zaidi uwanja huo utakavyojengwa.

"Tunashukuru Serikali ya Mkoa ambayo imetupa eneo la ujenzi wa uwanja, na baada ya taratibu zote ujenzi utaanza ili kuwapa fursa wananchi wa Mara kuwa na uwanja wa kisasa," alisema Bristow.

Aidha, alisema baada ya timu ya Biashara kushuka daraja, wananchi wa Mara hawana timu inayoshiriki mashindano maalum ya soka, hivyo kampuni hiyo imechukua jukumu la kuanzisha timu mkoani hapo.

"Pia tumeanza mchakato wa kuanzisha timu ambayo makazi yake yatakuwa mkoani hapa na ambayo itaungwa mkono na wananchi na wakazi wa mkoa huu," alisema Bristow.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanga, alisema shughuli za michezo mkoani humo lazima ziendelee licha ya timu iliyokuwapo mkoani hapo kushuka daraja.

"Kama wananchi wa Mara na serikali kwa ujumla tutaiunga mkono timu itakayoanzishwa, lakini tunaunga mkono ujenzi wa uwanja wa soka wa kisasa, tutawapa ushirikiano unaotakiwa," alisema Mtanga.

Aidha, alisema kuwapo kwa michezo endelevu kutawasaidia vijana kuepuka vishawishi vingi vinavyowapeleka kwenye matatizo ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya na wizi.

# Prisons kutangaza kocha mkuu leo, kambi Zanzibar

**Na Saada Akida**

KLABU ya Tanzania Prisons imesema baada ya kumpata kocha mkuu atakayekuja kukinoa kikosi cha timu hiyo, wataenda kuweka kambi visiwani Zanzibar kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa 2023/24 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Enock Manguku, alisema baada ya kuondoka kwa Kocha wao, Abdallah Mohamed 'Bares', wamelazimika kuendelea kusalia ndani ya kambi yao jijini Mbeya hadi hapo watakapokamilisha kumpata mrithi wake.

Alisema mipango yao ni kuweka kambi visiwani Zanzibar au jijini Dar es Salaam baada ya kukamilisha zoezi zima la usajili.

Manguku alisema kwa sasa timu imeanza kambi jijini Mbeya kwa muda wa siku kadhaa na leo wanatarajia kumtambulisha kocha mpya tayari kwa kukionGoza kikosi chao kuelekea msimu ujao.

"Tumejipanga vizuri kuanzia usajili na tayari baadhi ya wachezaji wetu wameanza kuingia kambini na muda wowote kuanzia leo tutaweka wazi majina ya wachezaji tuliowasajili pamoja na kocha wetu mkuu," alisema Manguku.

Aliongeza kuwa wako kwenye hatua ya mwisho ya mazungumzo na kocha huyo ambaye anakinoa kikosi cha timu hiyo kwa kutorudia makosa yaliyofanyika msimu uliopita ambayo yalisababisha kumaliza ligi kwa presha.

"Kila msimu ligi inakuwa na ushindani mkubwa, ukiangalia tumemaliza ligi tukiwa na presha kubwa ya kujinusuru kushuka daraja, jambo hilo hatuhitaji lijirudie katika msimu mpya, hivyo tutafanya usajili mzuri na kuimarisha benchi letu la ufundi,"alisema Manguku.



Robertinho

# Yanga yakubali kumuuza Mayele

INATOKA UK. 24

yaliyofikiwa ni nyota huyo kuuzwa," kilieleza chanzo chetu.

Hivi karibuni Mayele aliweka wazi kuwa atakuwa na mkutano wa mwisho na uongozi wa Yanga na Jumatatu (juzi), walikutana na kufikia maamuzi hayo.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Boniface Wambura, amesema kwa 'Status' ya Yanga Fifa inasomeka kuwa hawajafungiwa kusajili na kwamba klabu yoyote ikifungiwa taarifa hupitia TFF.

Alisema Yanga walikuwa wanadaiwa pesa na kocha wao wa zamani, Mbelgiji Luc Eymael, na wakazuiliwa kufanya usajili hadi wamlipe, lakini tayari walishakamilisha kumpa pesa zote alizokuwa anada.

"Tatizo lilikuwa kwenye 'email' (barua pepe), ambayo FIFA wamekuwa na mfumo mpya na pesa haikuingia kwenye 'system' (mfumo), kocha akaendelea kudai, lakini tulifanikiwa kutatua changamoto hiyo na kusajili hilo sasa ni jukumu lao Yanga," alisema Wambura.

Yanga tayari imemtambulisha mchezaji mmoja mzawa, Dickson Kibabage, akitokea Singida Fountain Gate FC na juzi Kocha wa timu hiyo, Miguel Angel Gamondi, alikutana na wasaidizi wake akiwamo meneja wa timu hiyo kwa ajili ya kuanza kazi rasmi.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema leo wanaanza mazoezi rasmi kujiandaa na msimu mpya wa mashindano yote ya msimu wa 2023/24.

Alisema katika programu ya kocha kuna ratiba mbili za mazoezi kwa siku, ambapo asubuhi watafanya mazoezi ya viungo katika gym za Gymkhana kabla ya jioni kufanya mazoezi ya uwanjani, kwenye Uwanja wa Avic Town, Kigamboni ilipo kambi yao.

"Kesho (leo), tunaanza rasmi mazoezi na yatakuwa mara mbili asubuhi na jioni ikiwamo ya utimamu wa mwili na jioni kiufundi na mbinu, Tunahitaji kuwa na msimu bora kama ilivyo kwa msimu uliopita, tunahitaji kuendeleza furaha zaidi kwa wananchi," alisema.

# Robertinho apagawa usajili

INATOKA UK. 24

Igendia akiwa na cheo kipya cha Meneja wa timu na Mkuu wa Sayansi ya Michezo, Kocha wa viungo, Corneille Hategekimana raia wa Rwanda, na Kocha wa Makipa, Daniel Cadena aliyekuwa kwenye klabu ya Azam, raia wa Hispania.

Wakati huo huo Simba iliondoka jana kuelekea Uturuki kwa kambi ya wiki tatu kujiandaa na msimu ujao ambapo Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kikosi hicho kimeondoka na wachezaji wote ambao wamesajiliwa, huku wale ambao bado hawajatangazwa wakitarajia kuungana na wenzao siku chache baadaye.

"Kikosi kimeondoka na wachezaji wote isipokuwa wale ambao hatujawatangaza, kuna mashine kama tatu nne hivi bado hazijatangazwa hadharani, lakini kwenye usajili tayari wachezaji wote ambao tuliwahitaji msimu huu tumekiwishawasajili, tutawatangaza na wengine watatoka hapa kuungana na kikosi Uturuki," alisema Ahmed.

Michezo

Jumatano Julai 12, 2023
Nipashe



## Kocha amtaka Kane asiondoke Tottenham

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakielekea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam tayari kwa safari ya Uturuki, kwenda kuweka kambi ya wiki tatu kujiandaa na msimu mpya. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAKUBALI KUMUUZA MAYELE

●●●Bilioni mbili za Wasaudia zatajwa, awekwa sokoni rasmi, ruksa sasa kusajili...

**Na Saada Akida**

BAADA ya juhudi za kumshawishi kuendelea kuitumikia timu yao kukwama, uongozi wa Klabu ya Yanga, umefikia makubaliano ya pamoja kumweka sokoni straika wao wa kimataifa, Fiston Mayele, imefahamika.

Mayele bado ambaye amebakiza mkataba wa mwaka mmoja, alikuwa kwenye mvutano na uongozi wa klabu yake kwa kufanya vikao kadhaa kabla ya juzi, Jumatatu kufanyika cha mwisho, lakini mshambuliaji huyo raia wa DR Congo akashilia msimamo wake wakuiomba Yanga kumuuza kwa moja kati ya klabu zinazomhitaji huduma yake.

Ingawa uongozi wa Yanga haukuwa tayari kuweka hilo bayana, chanzo chetu ndani ya kamati yao ya utendaji, kimelijuza gazeti hili kuwa wamefikia uamuzi wa kumuuza kutokana na msimamo wake.

Aidha, kilisema kwamba mbali na Klabu ya Zamalek, Pyramids (za Misri) na Esperance Sportive de Tunis kuonyesha nia ya kumsajili, pia kuna klabu moja ya Saudi Arabia ipo tayari kutoa Sh. bilioni mbili za Tanzania ili kuinasa saini ya nyota huyo aliyeongoza kwa ufungaji Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho Afrika.

"Ni kweli Mayele alikutana na viongozi juu ya mustakabali wake wa kuendelea kwa msimu ujao na makubaliano

UKURASA. 23

## Robertinho apagawa na usajili Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ameeleza kufurahishwa na wachezaji waliosajiliwa pamoja na benchi la ufundi, na kusema sasa kazi iliyopo ni kutengeneza kikosi imara ambacho anaamini kitawapa mataji mbalimbali msimu ujao.

Akizungumza jana kabla ya kupaa kwenda nchini Uturuki kwa ajili ya kuweka kambi, 'pre season' ya maandalizi ya msimu ujao wa mashindano, Robertinho alisema wachezaji waliosajili na wanaoendelea kuingia kwenye kikosi chake wametengeneza kitu ambacho alikuwa anahitaji siku zote kwa kila nafasi iwe na wachezaji bora kuanzia wawili ili kuleta ufanisi.

"Nimeridhika na kikosi changu, wachezaji wapya wanaosajiliwa ni wazuri hata wale waliopo wako imara, tunaamini maandalizi yetu yatakuwa mazuri nchini Uturuki, kuna wachezaji wengine wapya tutaungana nao tukiwa huko ili kukamilisha kikosi, msimu ujao tunahitaji kucheza vizuri na kushinda mataji, Simba ni timu kubwa na hilo lipo ndani ya uwezo wetu," alisema Robertinho.

Kuhusu benchi lake jipya la ufundi, kocha huyo raia wa Brazil alisema wote walioletwa wana wasifu mzuri na vigezo vyote, hivyo anaamini watafanya kazi zao vizuri.

"Makocha wote walioletwa wana wasifu mzuri, wana vigezo vyote vilivyoidhinishwa na mamlaka, naamini tutafanya kazi nzuri." alisema.

Tayari Simba imetangaza wachezaji wanne, watatu wakiwa wa kigeni na mmoja mzawa ambao ni beki wa kati Che Fondoh Malone, Mcameroon akitokea klabu ya Cotonsport ya nchini humo, winga na mshambuliaji msaidizi, Aubin Kramo Kouame kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast, naye akiwa ni raia wa huko, Willy Essomba Onana, anayecheza pia winga zote mbili na mshambuliaji msaidizi raia wa Cameroon akitokea Rayon Sport, pamoja na Mtanzania David Kameta akitokea Mtibwa Sugar.

Kwa upande wa benchi la ufundi, klabu hiyo imemtambulisha Mkenya Mikael

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >